BARAGUMU IKITOA SAUTI ISIYOJULIKANA

Asante sana, Ndugu Demos. Ni majaliwa makubwa kuwa hapa katika kusanyiko hili la Kikristo usiku wa leo, huku chini kwenye nchi hii iliyojaa barafu. Nami nilipiga simu nyumbani, muda mfupi uliopita, na ni karibu digrii ishirini joto zaidi, huko juu sana Kaskazini, kuliko ilivyo hapa chini. Lazima niliileta hiyo nilipokuja. Nitaharakisha nirudi tena, upesi sana. Mimea yote inagandamana. Unawazia nini kuhusu hilo, Creechy? Ni ninii . . . [Ndugu huyo anasema, "Ni baridi."—Mh.] Bila shaka ni baridi.

2 Pia nina furaha sana kukutana na mchungaji huyu mzuri, usiku wa leo, na kuwaona ninyi watu. Nimekuwa humu, dakika chache tu. Nimetoka Tucson, mahali iliponibidi kwenda leo. Niliteremka huko kwa gari jana usiku, nikafika kama saa nane na nusu usiku mapema leo, huko Tucson. Ndipo nikawa na shughuli siku nzima, kule chini. Kisha nikaondoka muda mfupi tu . . . Vema, nikaingia, imekuwa tu takriban saa moja u nusu, nadhani, kitu kama hicho, huku juu. Na kwa hiyo sijapata usingizi mwingi mno. Lakini nitajaribu nisishikwe na usingizi hapa. Lakini tuna—tuna furaha kuwa hapa.

3 Maskini mvulana huyu, anayecheza na maikrofoni hizi hapa. Niliketi chini nyuma kule, kwenye . . . kimoja cha viti vya watoto wadogo. Mvulana mdogo akaja, akaniangalia kigeni sana. Nikasema, "Sisi watoto wote tunaweza kuketi pamoja, sivyo?" Sasa, hakika ninawapenda hao jamaa wadogo, hata hivyo.

4 Na ni, loo, ni vizuri kweli kuwa hapa usiku wa leo, na kuwa na kusanyiko hili la kupendeza la watu wanaosimama kote huku. Nami nikitumaini sasa kwamba Ndugu Williams amewaambia yote kuhusu, na Ndugu Rose hapa, kuhusu mkutano ujao. Nadhani mnajua habari zake vizuri. Utakuwa huko Ramada, mara moja, mkutano wa Wafanyabiashara. Nasi tunatarajia wakati mkuu pale. Ndugu Velmer Gardner, mnenaji mzuri sana, hodari; na wahudumu wengine, Oral Roberts na wengi, watakuwa kule. Nasi tunatarajia wakati mkuu katika Bwana.

5 Natumaini, baadhi ya nyakati hizi, hebu na tufanye ibada ya uponyaji mahali hapo. A-ha. Ningetaka kumpata Ndugu Oral, nasi tukutane pamoja. Naam, bwana. Hilo si litakuwa ni sawa tu? Hilo lingekuwa ni u—ushindi mkubwa, sivyo? Ibada ya uponyaji, huko Ramada, hilo lingekuwa sawa. Sisi . . . Kwa hiyo huenda tukafanya hilo, mwajua. Huenda Bwana akatujalia hilo, tuwe na ibada ya uponyaji. Kwa hiyo tutaninii . . . Tunazunguka

sasa, kanisa kwa kanisa, kujaribu kueneza habari njema, na kujumuika mmoja na mwenzake, na kuwa na ushirika katika makanisa yote mbalimbali. Hilo ndilo tunaloamini, kwamba sisi ni mmoja, katika Kristo.

6 Nilikuwa nikizungumza hivi majuzi na daktari. Ninajiandaa kwenda katika nchi za ng'ambo, nawe huna budi kufanyiwa uchunguzi wa mwili. Kwa hiyo nilikuwa nifanyiwe uchunguzi. Basi akaniweka katika moja ya hayo mawimbi. . . Mimi. . . Msiniulize ni kitu gani. Ndipo akaona jambo la kigeni. Naye akarudi wala asingeweza kulielewa, ndipo akafanya baraza la madaktari, wala asingeweza kuelewa hilo. Akasema, "Sijawahi kuona hilo hapo kabla." Na kwa hiyo akanionyesha picha yake, jinsi ambavyo ambapo dhamira ya kawaida, nawe una dhamira ya ndani, nazo ziko mbali sana moja kwa nyingine. Lakini akaona kwenye yangu zote mbili zilikuwa pamoja. Kasema, "Wewe ni jamaa wa kipekee kweli."

Nikasema, "Sikuzote nimejua hilo. Kila mtu anajua."

7 Kasema, "Hatujawahi kuona hilo hapo kabla." Kwa hiyo akaanza kuniambia habari zake.

8 Nikasema, "Vema," nikasema, "unajua, nadhani Bwana mwema, anapotufanya, Yeye hutufanya tu tofauti kidogo. Hatufanani, na kwa hiyo wakati mwingine hata hatutendi sawa na mwingine. Lakini—lakini Yeye hulifanya Kwake, njia Yake ya kulifanya. Tunaingia tu kwenye mtambo mkubwa wa kufinyanga, nasi tutakaa tu kimya, Yeye atatufinyanga jinsi anavyotaka tuwe."

9 Na mimi—mimi ninajua hakuna mtu angetaka kuwa chochote ila kile ulicho. Jambo pekee sisi sote tunaloweza kutamani. . . Tukiisha kuokolewa na kuwa watoto wa Mungu, jambo pekee tunalotaka ni kutembea karibu zaidi kila siku. Hilo ndilo tunalotamani, kwa ajili ya ushirika huo mkuu. Jinsi lilivyo la ajabu! Ungeweza kamwe kutulia na kuwazia yale ambayo tungefanya kama hatukuwa na hilo? Vipi—vipi. . . Kama hilo tumaini kuu halikukaa ndani yetu, tungefanya nini?

10 Nilikuwa nikisema, katika moja ya makanisa, hebu mimi. . . Kwanza, mahali pamoja, kisha pengine, na kote nchini ninatoa tamshi wakati mwingine, nawazia huenda nikalirudia katika kanisa lilo hilo. Lakini nilikuwa nikitoka nje ya jengo ambako kidogo nilikuwa nikihubiri kwa ukali sana, kuhusu watu hawa siku hizi wanaocheza dansi hii mpya waliyo nayo, wanaiita twisti, ama kitu fulani. Ndipo nikasema, "Sijui kabisa, kile hasa, watu wanataka kuvunjia miguu yao na—na kutenda hivyo."

11 Kwa hiyo, kulikuwako na jamaa mmoja, mwenye umri wa kama miaka ishirini na sita hivi, ishirini na saba, aliyekutana nami huko nyuma, kasema, "Hebu kidogo, Bw. Branham."

Nikasema, "Naam, bwana?"

Yeye akasema, "Unajua, kamwe huelewi."

Nikasema, "Natumaini kamwe sitaelewa."

12 Kwa hiyo akasema, "Unaona," akasema, "Ninaweza kuona hoja yako." Kasema, "Wewe ni mtu mwenye umri wa miaka hamsini. Lakini kama ulikuwa wa umri wangu, ingekuwa ni tofauti."

13 Nikasema, "Ngoja kidogo." Nikasema, "Nilikuwa nikihubiri Injili nilipokuwa miaka kumi mdogo kuliko ulivyo wewe. Ningali ninaiamini Injili iyo hiyo. Nilipata kitu kinachopachukua mahali hapo, na furaha zaidi katika kumtumikia Bwana kuliko mambo yote ambayo ibilisi angeweza kubuni mahali popote." Ni ninii . . . Linaleta kuridhika.

14 Mwajua, Daudi alisema, wakati mmoja, "Kama vile ayala aoneavyo shauku mito ya maji, nafsi yangu inakuonea Wewe kiu, Ee Mungu."

15 Na kama ulipata kumwona mmoja wa jamaa hao wadogo, wakati yeye ame—amejeruhiwa; labda mbwa wamemshika, na kung'wafua kipande kikubwa kutoka ubavuni mwake, ama kitu fulani. Anatokwa na damu. Basi, yeye, mbwa anaweza kumwandama. Yeye si kama mwanadamu. Naye anaweza kumwinda kulungu huyo kama anatokwa na damu ama sivyo. Na kwa hiyo njia pekee . . . Kama kulungu huyo anatokwa na damu, jinsi tu anavyoweza kuishi ni kufika palipo na maji. Na kama anaweza kufika palipo na maji, yeye atayanywa maji hayo. Yataukomesha mtiririko wa damu, na—naye anaweza kutoroka. Ni mwerevu sana.

16 Lakini sasa mnaweza kuwazia, mkimwona mmoja wa jamaa hao wadogo amejeruhiwa na anatokwa na damu, na jinsi ambavyo anakiinua tu maskini kichwa chake juu, na hisi zote alizo nazo za kugundua mahali yalipo maji, kwa pua yake. Ninii tu, hana budi kupata maji, la sivyo aangamie. Na sasa ni kufa na kupona, kwake yeye. Yeye, kila tu—kila—kila moja ya hisi alizo nazo, yeye anajaribu, ana shauku. Hana budi kuyapata.

17 Sasa, hivyo ndivyo tunavyopaswa kuwa tukimwonea Mungu kiu. Mnaona? "Kama vile ayala aioneavyo shauku mito ya maji, nafsi yangu inakuonea Wewe kiu, Ee Mungu." Kufichwa pamoja na Yeye mahali fulani, ndiyo shauku ya moyo wangu. Nami ninatumaini ya kwamba hiyo ndiyo shauku ya wote walio humu ndani usiku wa leo.

18 Na sasa, usiku baada ya usiku, nami ninapenda kuliona hili. Nyuso unazoona mahali pamoja, unaziona mahali pengine. Na—napenda hilo. Ninyi kuonyesha ushirika wenu, na kuonyesha kile kilichotuleta hapa.

19 Na, loo, hakika ningetaka kuona uamsho wa mtindo wa kale katika Phoenix. Loo, jamani! Neno hilo *Phoenix* limenichangamsha tangu mara ya kwanza niliposoma habari

zake, zake: Phoenix, Arizona. Jamani, maskini mvulana mdogo, niliwaza, “Laiti ningaliweza kupafikia mahali pale! Laiti ningaliweza kufika kule, Phoenix!” Na sasa naiona, na wakati tukiwa hapa tunaikuta imedidimia katika kilindi cha dhambi, kama mahali pengine pote, watalii wakiingia kwa wingi; na kunywa pombe, karamu za ulevi, utovu wa uadilifu, na kila kitu kipo.

20 Lakini, hata hivyo, katikati ya hayo yote, unakuta lulu zingine halisi ambazo Mungu alitikisa kutoka kwenye jangwa hili hapa, zinazong’ara katika taji ya watu wa Mungu waliotukuka. Na hilo ndilo lililonileta hapa, usiku wa leo, kujiweka mwenyewe pamoja nanyi enyi ndugu na nyinyi akina dada, kujaribu kuwaangazia wengine Nuru ya Bwana Yesu, waweze kupatikana, pia, katika machafuko haya makuu. Na wengi wao wako huko nje bado. Ninaridhishwa na hilo. Kungali na wengi watakaoingia, nasi hatuna budi kufanya kila kitu tuwezacho tuwapeleke kule, na kuishi maisha yatakayomwakisi Kristo.

21 Sasa, kabla tu hatujasoma somo dogo la Maandiko... Niliingia nimechelewa sana nikaandika muhtasari kidogo, katika dakika kama tano. Na idara ya kodi ya mapato ya shirikisho ndio kwanza wanitumie ripoti fulani, ilinibidi kuingia mara moja, nayo haina budi kuidhinishwa, nafikiri, labda leo, bado. Na kwa hiyo ikanibidi kwenda kwenye posta. Ndipo nilipoingia, Billy alisema, “Afadhali uharakishe.” Na kwa hiyo hapa...

22 Nilikuwa tu nimezunguka, na kuzunguka, kuzunguka, na jamaa hao. Jamani, loo, jamani! Wananena kuhusu haki milangoni mwa mahakama. Nashangaa iko wapi. Naam. Sijaona kitu kama hicho. Nao walinitaka nilipe kodi ya mapato kwa kila hundi ambayo nimepewa kwa miaka hamsini iliyopita, kulipia madeni ya uamsho, pamoja na ushuru uliochelewa juu yake, mnaona, dola mia tatu hamsini na tano elfu.

23 Nikasema, “Nipigeni risasi tu.” Ningewezaje kufanya hivyo? Nikasema, “Sina angalau senti hamsini na tano.” Nikasema, “Ningewezaje kamwe kufanya hivyo?” Nao wamenisumbua vibaya sana kwa miaka mitano.

24 Kwa hiyo, juu ya matoleo ya watu. Tuseme, tunafanya uamsho, na—nao watu, wanajua tu jina langu ni William Branham, wanaandika tu hundi kwa ajili ya matumizi. Wahudumu wanashughulikia hayo. Kamwe sijachukua matoleo maishani mwangu. Na kwa hiyo wanachukua...Mimi hupata m—mshahara kutoka kanisani mwangu, dola mia moja kwa juma.

25 Nayo matoleo haya...Lakini kila mmoja, mnaona, kwamba wanachangia hayo...Basi kesho yake asubuhi, yu—yu—yu—yule aliyekuwa mkubwa wa kamati ya fedha, angekuja huko

na kusema, "Ndugu Branham, inakubidi kutia sahihi hundi hizi." Na, mbona, ningezitia sahihi tu. Naye angeziweka mle. Ndipo wao wakachunguza hizo zote, na hakuna hata senti moja iliyotumika kwangu binafsi. Lakini nilipoitia sahihi hundi hiyo, wao walisema ilikuwa ni yangu. Ati hao watu walinipa, kisha nikalipa kanisa. Loo, jamani!

26 Nilijisikia vibaya sana, mara ya kwanza, ndipo nikaja kutambua kwamba kila mtu katika Biblia, naamini, aliyewahi kuwa na ofisi ya kiroho kwa Mungu, alihusishwa na serikali za shirikisho. Chunguzeni muone. Hiyo ni kweli. Musa, Danieli, Yohana Mbatizaji. Yesu Kristo alikufa kwa mkono wa serikali ya shirikisho, chini ya adhabu ya kifo. Petro, Yakobo, Yohana, Yohana mfunuzi, wote, kila . . . Wote walipata mateso.

27 Kwa nini? Ndicho kiti cha Shetani. Mnajua hilo? Mnajua, Shetani alimpandisha Yesu na kumwonyesha falme zote, ulimwengu, kwa dakika moja? Naye akasema, "Zote ni zangu. Mimi hufanya nazo lolote nitakalo. Mnaona? Nami nitakupa Wewe kama utaanguka chini na kunisujudia." Kwa hiyo unaona kwamba ni za nani? Tunachukia kuwazia hilo juu ya yetu, bali ni yake.

28 Kwa hiyo Yeye akasema, Yesu akasema, "Rudi nyuma yangu, Shetani." Yeye alijua atazirithi, katika ule Utawala wa Miaka Elfu. Yeye alijua zitakuwa ni Zake wakati . . . Ambapo, kama nchi hizi zilitawaliwa na Mungu, ule Utawala wa Miaka Elfu ungekuwa unaendelea. Lakini kutakuwako na wakati.

29 Wana U.N. na Mashirikisho ya Mataifa, na kila kitu, kujaribu kuleta amani. Lakini mradi tu Shetani yuko juu yake, na siasa, kutafanyika nini? Hakika watapigana.

30 Bali utakuja wakati ambapo silaha zote zitawekwa kando. Navyo ving'ora vitalia, nayo asubuhi itapambazukia Umilele, angavu na dhahiri. Mfalme wetu atachukua Kiti Chake cha Enzi. Loo! Kutakuwa na kuimba; kutakuwa na kupaza sauti. Na kutakuwako na bendera moja, watu wamoja, taifa moja, likizungumza lugha moja, ya Kimbinguni. Amina. Ninatamani wakati huo. Nami ninakaza mwendo niifikie mede hiyo, nikimtumaini Mungu, siku moja wakati imekwisha, ninaweza kusema . . . Ninaweza kumsikia Yeye akiniambia, "Njoo huku juu zaidi."

31 Niko hapa Phoenix usiku wa leo katika Jina la Bwana. Ninge—nisingejaribu kuelezea yale yaliyotukia. Wengi wenu ninyi watu mnaozichukua hizi kanda, hakikisheni mtaipata hiyo, *Ni Wakati Gani, Bwana?* Hiyo ilikuwa tu kabla sijaondoka nyumbani. Ono lilinituma hapa; ni, sijui nini . . . Sijui . . . Mimi si mwuza kanda, wala siyatilii mkazo mambo hayo. Tunazipata, nasi tuna kazi ya kanda kote ulimwenguni. Huko mbali katika misitu na kila mahali, wana kitu fulani kidogo wanachotia maskioni, wanacho, nao wanaweza kuunasa katika kanda, na

kusimama pale na kuufasiri huo moja kwa moja katika lugha yao. Nao unaenda kote ulimwenguni.

32 Na, lakini mmoja niliokuwa nao, huo *Ni Wakati Gani, Bwana?* Ama, *Je! Huu Ndio Ule Wakati, Bwana?* Baadhi... Mimi...Jumamosi usiku, majuma matatu yaliyopita, huko kanisani. Baada ya maisha yangu yote ya kuona maono, kamwe sikupata kuwa na kitu kama hiki hapo kabla, maishani mwangu. Wala sijui ni kitu gani. Mimi nipo tu hapa, bali Yeye alinituma hapa. Sijui inamaanisha nini. Ninaninii tu... Nipo tu hapa.

33 Nami sina budi kuwa mwaminifu na mkweli, na hivyo ndivyo tu tutakavyoweza kufikia mahali popote na Mungu, ni kuwa mwaminifu. Maana, watu watajua. Mungu anajua, hapo mwanzo, sivyo ulivyo, kama ndivyo ulivyo ama sivyo. Nao watu watajua. Kwa sababu, wakati mmoja, kulikuwa na mtu aliyekuwa akijaribu kutabiri. Naye Mungu akamwambia... Ama, yule nabii halisi akamwambia, kasema, "Hebu tukumbuke. Kumekuwa na manabii mbele yetu. Nabii anajulikana tu wakati unabii wake unapotimia." Kwa hiyo ni afadhali tuwe na hakika kwamba tunajua Mungu alisema hivyo, kabla hatujasema lolote kulihusu. Kuwa mwaminifu na mkweli.

34 Sasa hebu na tuviinamishe vichwa vyetu kwa muda mfupi tu kwa ajili ya maombi. Sasa hebu na tuweke kando kila mzigo sasa, kwa dakika chache zijazo. Sijui... Katika kundi hili dogo la kupendeza la watu hapa usiku wa leo, ninajua kwamba kunazo hizo lulu zinazoketi hapa ambazo Yesu atakuja kuzichukua siku moja, ambazo zitafufuka kutoka mavumbini.

35 Na huenda kukawa na wengine hapa wasio na hakika sana kama watakuwa kule, au hawatakuwa. Huenda ikawa mna haja ya vitu vingine. Iwapo kuna haja maishani mwako usiku wa leo, acha ijulikane kwa Mungu, unapoinua tu mkono wako, ukisema tu, "Mungu, Wewe unajua ninalomaanisha sasa. Na unibariki. Mimi, mimi ni mgonjwa. Ninahitaji uponyaji. Mimi—mimi ni mkaidi. Ninahitaji kurudi kwenye ushirika. Na—nataka kurudi. Ni—nimekosea. Ninarudi. Ninakutaka Wewe unisaidie, usiku wa leo, nipate kurudi." Mungu akubariki.

36 Baba wa Mbinguni, sasa wakati tukikikaribia kiti Chako cha enzi, kwa njia ya Damu. Kwa kuwa... Naye Aaroni alienda mbele ya ki—kiti cha rehema, akachukua, kwanza, damu mkononi mwake, naye akaenda mbele. Nasi, kwa imani usiku wa leo, tunaipokea Damu ya Yesu Kristo, na kutembea kuelekea kwenye kiti cha enzi cha Mungu, kwa ujasiri, tukijua ya kwamba tunayo haki kuja, sio katika haki yetu wenyewe, bali katika Yake. Damu inawakilisha kutakaswa kwetu. Nami ninaomba, Baba wa Mbinguni, ya kwamba Wewe utatujalia maombi yetu.

37 Kwanza, tungekuomba Wewe uturehemu, ukitusamehe makosa yetu yote, tunapokiri makosa yetu, na makosa yetu

madogo, na dhambi zetu za kisiri, na dhambi zetu zisizojulikana. Nasi tunakiri pia kama wahudumu, tukiwa makuhani, dhambi za watu. Pamoja, Bwana, tunasimama. Tunawapenda watu. Tunajisikia kama Musa wakati alipojitupa katika pengo, kuwashikilia watu, hasira ya Mungu. Lilikuwa ni onyesho la jinsi gani hilo, la haki ya Kristo, hapo Kristo alipojitupa Mwenyewe katika pengo, apate kuwaokoa watu.

38 Pia, Baba, sisi kama watumishi Wake, pamoja na Roho Wake ndani yetu, kila Mkristo hapa ndani usiku wa leo, anajishikilia mbele ya mwenye dhambi: "Mungu, warehemu." Tunawalilia wagonjwa na wahitaji, kwa ajili ya mikono hiyo ya thamani, baadhi yao ni wazee, na wengine vijana, na wengine ni wa umri wa makamu, wanaoinua mikono yao. Unajua yote kulihusu, Bwana. Tunaomba ya kwamba Wewe utajibu kulingana na utajiri Wako katika utukufu.

39 Jalia kuwe na wengi usiku wa leo, Bwana, watakaotoka hapa, walioingia, ambao ni wagonjwa, jalia waondoke, wazima, wameponywa. Kitu fulani ndio kwanza kitukie, hata hawawezi kukielezea, bali wanajua ya kwamba ni wazima.

40 Jalia walio wakaidi waondoke wamehesabiwa haki, Bwana, tukijua ya kwamba wamerudi na kumchukua Kristo mahali walipomwacha. Jalia waende, wakafanye upatanisho. Tujalie, Bwana, kwamba wale ambao hawajawahi kuja watapata ule uhuru wa thamani wa kuwa huru, kutolewa kwenye kizimba, hawafungwi tena na mambo ya ulimwengu na shughuli za maisha haya, bali wamefanywa huru katika Kristo. Tujalie, Baba.

41 Bariki yote tunayohitaji sasa, na ulibariki Neno Lako na mtumishi Wako, nasi tutakupa Wewe sifa. Katika Jina la Yesu tunaomba. Amina.

42 Sasa, kama tungesoma somo la Maandiko, ama Maandiko kwa ajili ya somo, hasa, Wakorintho wa Kwanza mlango wa 14, kifungu cha 8, inasoma hivi, katika Wakorintho wa Kwanza 14:8.

> *Kwa maana baragumu* ikitoa *sauti isiyojulikana, ni nani atakayejifanya tayari* kwa ajili ya *vita?*

43 Hili lingekuwa ni somo la kutosha ambalo tungekuwa tukihubiri majuma mawili tangu sasa juu yake, na hata hivyo tusiguse kingo zake. Kuna kitu fulani kuhusu Neno ambalo limetiwa pumzi. Sikuzote uko kwenye fungu hilo moja. Unaweza kuifunganisha Biblia nzima nalo. Hiyo ni kweli.

44 Siku moja jamaa fulani aliniuliza, kasema, "Unawezaje kuchukua fungu lile lile?"

Nikasema, "Loo, jamani! Unachukua muktadha wa chochote kutoka kwake."

45 Niliokota klova ndogo ya majani matatu iliyokuwa ardhini, na kuiinua juu. Mtu huyo ameketi hapa usiku wa leo, kutoka

Tucson. Nasi tulikuwa huko Pasadena, California. Ndipo nikasema, “Ningeweza kuchukua klova hii yenye majani matatu na kuhubiri miaka ishirini na mitano juu yake: jinsi ambavyo ni uhai, uliomo ndani yake; jinsi ambavyo, hayo majani matatu, yakiwa ni utatu katika Mmoja. Na, loo, loo, kuna mambo mengi tu ambayo tungeweza kusema juu yake.”

46 Basi vipi kuhusu Maandiko? Ni Neno la Mungu. Ni ya Milele. Ni—yalikuwa . . . Hayana mwisho. Linazidi tu kuendelea mbele, zaidi, zaidi. Ni kimbilio kwetu.

47 Na sasa usiku wa leo ninataka kuzungumza juu ya hili: *Baragumu Ikitoa Sauti Isiyojulikana.*

48 Katika kuwazia hilo, muda mfupi tu uliopita, nilipokuwa nikiwazia juu ya . . . lile suala la ushuru wa mapato, nikawaza, “Karibu hakuna chochote siku hizi kilicho na uhakika. Kila kitu kina mashaka mengi sana kwake.” Na chochote kilicho na mashaka hakiwezi kuaminika. Chochote kisicho na uhakika hakiwezi kuaminika. Kaa mbali nacho kama hakina uhakika.

49 Iwapo una biashara; na, ambayo, tuna wafanyabiashara waliopo hapa, labda wengi wao. Ikiwa unaendesha biashara ambayo haina uhakika, hutawekeza sana ndani yake, kwa sababu m—mgawo wake wa faida hauna uhakika, nawe hutawekeza sana humo. Ama, kama wewe ni mfanyabiashara mzuri, mwerevu, utangojea na kuchunguza, ikiwa una fedha za kuwekeza, mpaka upate kitu ambacho kina uhakika, kitu ambacho ni cha kutegemewa, kitu ambacho unaweza kukitegemea. Kwa sababu, hutaki kupoteza pesa hizo kidogo ambazo umeweka akiba, kwa sababu kwa hizo huna budi kupata riziki yako, kutokana na mapato kutoka—kutokana na mgawo wa faida iliyotoka kwenye uwekezaji huu. Mbona, huna budi ku—kupata kitu cha kuishia.

50 Na pesa hizi kidogo ulizoweka akiba, usiziweke mfukoni mwako na kuziacha mle, kwa sababu wezi wataziiba. Unaona? Usifanye, usifanye hivyo. Kama unazo, ziwekeze katika kitu fulani. Halafu unataka kuwa na uhakika na uwekezaji wako. Usipokuwa nayo, mbona, kamwe usiiwekeze, hata kidogo.

51 Kwa hiyo, biashara hakika iko katika msimamo usio thabiti usiku wa leo. Biashara yoyote, karibu yote, ulimwenguni, iko katika hali ya udhaifu, kwa sababu ulimwengu uko katika hali ya udhaifu. Huwezi tu kujiachilia . . .

52 “Sasa, nitaweka akiba fedha *kiasi fulani*, nikajijengee maskini makazi mazuri, mahali fulani.” Hiyo ni, hiyo haina uhakika kabisa. Nitakwambia haina, kwa sababu huenda serikali ikaichukua yote, kwa ghafla.

53 Loo, mambo ambayo yemeifanya demokrasia yetu kupotoka sana, hata si imara tena! Ilikuwa tungeweza kuweka matumaini mengi sana katika demokrasia yetu. Na, ambayo, kweli nadhani ndio aina nzuri kuliko zote za serikali. Lakini, hata hivyo,

demokrasia yetu si imara. Kwa sababu, sisi, taifa hili, watu wetu, tunayo katiba, na katiba hii ndiyo—ndiyo yakini yetu. Lakini, hata hivyo, katika hilo, katiba yetu si imara, kwa sababu tayari imevunjwa mara nyingi. Hayati Bw. Roosevelt aliifanyia uharibifu mkubwa. Kwa hiyo, mnaona, mnaona inaweza kuvunjwa. Hamna matumaini makubwa unayoweza kuweka ndani yake.

54 Siasa, loo, jamani, jinsi zisivyoaminika! Watu wanabishana tu, na kubishana, na kubishana, juu ya siasa. Nao majirani watakosana, juu yake, na watu ambao wakati mmoja walikuwa ni marafiki wazuri. Rais fulani atainuka, ama mtu fulani, kugombea uliwali, ama kitu fulani, naye jamaa huyo mwingine upande wa pili wa uzio wa kisiasa, nao watabishana mmoja na mwenzake mpaka wakosane juu yake, siasa. Nami sininii... natumaini siumizi hisia za mtu yeyote, bali nafikiri kitu hicho chote kimeoza. Mnaona? Naam, bwana. Kwa hiyo kwa nini kubishana na kukosana juu ya kitu ambacho si kizuri kwa vyovyote vile? Hiyo ni kweli. Ni vibaya tu sana.

55 Mtu fulani aliniambia hivi majuzi, akasema, "U—utapiga kura kwenye uchaguzi huu?"

Nikasema, "Tayari nimepiga kura."

Kasema, "Loo, kwenye uchaguzi huu?"

56 Nikasema, "Nalimpigia kura Yesu." Nikasema, "Nitakwambia. Kulikuwa na watu wawili walionipigia kura." Nikasema, "Mungu alinipigia kura, naye ibilisi akapiga kura dhidi yangu. Nami nikampigia Mungu kura, kwa hiyo nilipiga kura yangu vizuri." Inategemea unapiga kura yako wapi, jinsi utakavyotokea.

57 Kwa hiyo, angalieni, hivi majuzi tu, kuwaonyesha tu mahali padogo, kisha tutaliacha. Katika uchaguzi huu wa mwisho wa rais, wakati ilithibitishwa kabisa huko Chicago na mahali mbalimbali, kwamba ile mitambo waliyotumia kupigia kura, kwamba, ilikarabatiwa na chama cha Democratic, kwamba kila ulipompigia kura Bw. Nixon, ilikubidi kumpigia kura Bw. Kennedy, wakati uo huo. Kwa hiyo, huna bahati. Na ilithibitishwa!

58 Nanyi mlilisikia *Monitor* hivi majuzi usiku, wakati walipofanya u—uchunguzi kote nchini, kutoka Mississippi, mashariki. Bw. Nixon alikuwa amepata kura hizi za kupiga simu, nne kwa moja. Mtu anawezaje kushinda? Kama ingalikuwa ni Bw. Kennedy, ingalikuwa ni vile vile. Mimi sina chama chochote.

59 Chama changu kiko Mbinguni, nami niko papa hapa pamoja nao usiku wa leo. Tumeketi katika mahali pa Mbinguni, tukizungumza habari za Mfalme wetu.

60 Lakini, mnaona, ninajaribu kuwaambieni, mambo haya ya duniani yanatikisika. Hapo, huwezi kuweka matumaini yoyote kwao. Hayaaminiki. Na chochote kisicho imara, ni afadhali nikiache tu. Sipendi kitu hicho kibaya. Sipendi kujichanganyisha na upande mbaya. Napenda uhakika, kuwa upande mzuri.

61 Sasa, maisha ya kinyumbani yamekuwa hayana uhakika. Mwajua, niliona makala hivi majuzi, katika moja ya majarida mahali fulani, kwamba kiasi cha talaka Marekani kiko juu kuliko taifa lingine lolote ulimwenguni. Nasi tunadhaniwa kuwa ni taifa la kidini. Naam, yaweza kuwa, dini, vema, bali si ile sahihi. Mnaona? Dini ni kifuniko tu. Ni vigumu kujua tunachotumia kufanya kifuniko chetu. Adamu alijaribu kufanya baadhi kutokana na majani ya mtini, na havikufanya kazi. Kilikuwa dhaifu sana wakati ilipombidi kuja kukutana na Mungu. Kwa hiyo dini haitoshelezi hata kidogo. Lakini ungeweza kuwazia kwamba kiwango chetu cha talaka, ni cha juu kuliko—kuliko nchi zingine zote, kiwango chetu cha talaka? Tunaona utovu wa uadilifu ukiingia katika nyumba zetu.

62 Lilikuwa ni la kushangaza sana kuona, kwamba, sehemu kubwa ya ule uchunguzi wa taifa. Na katika . . . Ninaamini ilikuwa ni Ohio, ambapo Ukristo ulifanyiwa uchunguzi, na ilishtusha kwamba ni asilimia ngapi ya wale ambao hata hawaendi kanisani. Halafu basi, yapata asilimia themanini ya wale wanaoenda kanisani, hawakujua ni kwa nini walienda. Hawajui ni kwa nini wanaenda. Wanaenda tu kanisani.

"Wewe huenda kwa nini?"

63 "Vema, mama alitupeleka tulipokuwa watoto wadogo, nasi tunaendelea tu kwenda." Na—na halafu, sasa, asilimia nyingine ya hao, ilisema walienda tu kwa ajili ya, loo, kukutana na majirani zao na kuzungumza kidogo. Mnaona?

64 Mbona, linashangaza sana! Si ajabu maisha ya nyumbani yamekwisha, mnaona, maisha yoyote ya nyumbani yasiyo thabiti.

65 Mwanamke yeyote anayeelekea kuolewa na mwanamume, naye hana uhakika na mwanamume huyo, afadhali amwache. Pia mwanamume yeyote anayetaka kumwoa mwanamke, wala hana uhakika, heri uachane naye. Afadhali uombe mpaka ujibiwe, juu yake, mpaka Mungu akupe jibu. Halafu anachokiunganisha Mungu mwanadamu yeyote asikitenganishe. Lakini sisi—sisi, kwanza, hatuna budi kuomba mpaka tujibiwe, juu ya hilo. Naam.

66 Sasa, tunaona ya kwamba tumejaribu kuuongoa ulimwengu kwa mfumo wa elimu, nasi kweli tumechafua yote, hakika kabisa. Huwezi kuuongoa ulimwengu kwa Kristo kupitia elimu. Elimu inamwondosha kwa Mungu, kuliko vile inavyomvuta kwa Mungu, kwa sababu yeye hujaribu kufikiria ni mwerevu

zaidi na anajua zaidi kuliko mtu mwingine. Kadiri elimu ilivyo nzuri, Kristo kamwe hakuliagiza kanisa Lake kuuelimisha ulimwengu. Kamwe Yeye hakuwaelimisha, kufanya seminari. Kamwe hakuwaeli-. . . Loo, ni nzuri. Kamwe hakuwaambia waende wakajenge hospitali. Hilo ni sawa.

67 Lakini jukumu la Kanisa ni kuihubiri Injili. "Enendeni ulimwenguni kote, mkaihubiri Injili kwa kila kiumbe." Mnaona? Lakini lolote tofauti na hilo, linakuwa si thabiti, kwa sababu liko nje ya mpango wa Mungu.

68 Maisha ya kitaifa si thabiti. Vema, ulimwengu si thabiti. Tunaishi tu mahali ambapo ulimwengu mzima una wasiwasi mkuu, inavyoonekana, ukiwatikisa wote. Kila taifa, kila mtu, mmoja anamwogopa mwenziwe. Wanazungumza amani.

69 Walikuwa, wakati mmoja, wao walisema, "Loo, tutakapomaliza Vita vya Kwanza vya Dunia, kwamba wavulana wetu wote hawana budi kwenda kule, na hiyo itamaliza vita vyote." Mbona, hata hawakuwa wameupulizia mbali moshi wa ile mizinga mikubwa hewani kabla hawajaingia katika vita vingine.

70 Halafu wakawa na Shirikisho la Mataifa, na hilo lilikuwa liulinde ulimwengu, nalo likashindwa vibaya. Sasa wana U.N., na ni kitu kile kile hasa. Tayari umeshindwa kabisa. Haufai kitu.

71 Kila kitu kinayumbayumba; maisha ya taifa, maisha ya kisiasa, mitambo ya kupigia kura. Loo, jamani! Wananinii tu . . . Kitu hicho chote kimetikisika, kila kitu.

72 Sasa ninataka kulileta kidogo karibu na nyumbani. Mnaona? Maisha ya kanisa ni dhaifu na hayaeleweki. Sasa, hilo ndilo Paulo alilokuwa akizungumzia. Mnaona? Hapo ndipo alipomaanisha, "Baragumu ikitoa sauti isiyojulikana." Maisha ya kanisani yamevurugika. Watu karibu hawajui la kufanya. Wanaenda, wakitangatanga kutoka kanisa moja hadi lingine, wakijaribu kutafuta ni lipi lenye kitu cha kweli; wakienda huku na huku, wakijaribu kutafuta yaliyo sahihi, mahali palipo na fundisho la kweli. Basi mmoja atakuja huku, nao wanaweza kulielezea, karibu tu kufikia hoja yenyewe ya kanuni ya imani yao, ni kweli. Halafu basi, muda si muda wajua, wanapata upotovu mwingi sana katika hilo, hata wanajaribu kanisa lingine, waone kanuni yao ya imani ni nini, fundisho. Loo, yote haya, tunaona ya kwamba tumejivunja-vunja basi, kwa mambo haya, katika mamia ya taratibu mbalimbali za kanisa. Sasa, hakuna kitu dhidi ya hilo. Hiyo ni kwamba tu wanaweza kufanya hayo mambo mengine, basi, wafanyayo, na hapana budi pawe na matokeo mazuri kwake, mahali fulani.

73 Ila, unaona, huwezi kuweka matumaini yako katika kusema, "Mimi ni mfuasi wa shirika la makanisa ya Methodisti, na mimi—mimi niko sawa kwa sababu ni mfuasi wake." "Mimi—

mimi—mimi ni mfuasi wa shirika la Kibaptisti, nami niko sawa.” Huwezi kufanya hilo.

74 Hata huwezi kulifanya wakati unaposema wewe “ni mfuasi wa shirika la makanisa ya Kipentekoste.” Huwezi kufanya hivyo. Haikupasi kufanya hivyo, kwa sababu sivyo. Tunaona ya kwamba wakati shirika letu la kwanza la Kipentekoste, lile Baraza Kuu, lilipoundwa, haikuchukua muda mrefu sana kabla hawajaanza kutengana kutoka huko, na kutengana kutoka hapa, na hoja, na mafundisho. Na sasa liangalieni tu, kila mahali. Mnaona? Inaonyesha ya kwamba halina msimamo. Wale wanaotumainia tu dhehebu pekee, si—si imara.

75 Sasa, ungesema, “Ndugu Branham, unatutilia chumvi sana hapa. Unachora picha ya giza ya kutisha sana.” Na ninakusudia kufanya hivyo. Nilitaka kufanya hilo.

76 Nilifanya hivyo makusudi, nipate kusema hivi. Kuna chochote kilicho cha hakika? Naam. Kuna kitu kimoja kilicho cha hakika. Loo, nina furaha sana kwa ajili ya hilo, kwamba kuna kitu kimoja unachoweza kukitumainia, na kuwa na hakika kwamba ni cha kweli. Loo, wakati kila kitu kingine kimekwisha, *Hili* litakuwa limesimama. Iwapo utasoma Mathayo Mtakatifu 24:35, Yeye alisema, “Mbingu na nchi zitapita, bali Neno Langu halitashindwa.” Mungu anao msingi imara.

77 Mzee mmoja, alisema wakati mmoja, mzee mweusi huko Kusini. Alibeba Biblia, wala asingeweza kuisoma. Nao wakasema, “Kwa nini unaibeba, Sam?”

78 Yeye akasema, “Ni—ni Biblia Takatifu.” Kasema, “Imeandikwa juu yake.” Kisha kasema, “Ninaiamini, kutoka jal’da hadi jal’da, nami naamini jal’da pia,” akasema, “kwa sababu ina ‘Biblia Takatifu’ imeandikwa juu Yake.”

79 Naye jamaa huyo aliyekuwa akisemezana naye, kasema, “Huamini yote yaliyo ndani Yake?”

Kasema, “Naam, bwana. Hakika ninaamini.”

80 Akasema, “Sasa, vema, unamaanisha ungefanya lolote Biblia hiyo ingesema ufanye?”

Akasema, “Naam, bwana.”

81 Kasema, “Vipi kama Biblia hiyo ilisema Sam aruke kupitia *ule* ukuta wa mawe pale? Ungefanya nini?”

Akasema, “Ningeruka.”

82 Akasema, “Vema, sasa, utapitaje kwenye huo ukuta wa mawe pasipokuwapo na shimo mle?”

83 Akasema, “Iwapo Biblia ilisema Sam aruke, kungekuwako na shimo pale wakati Sam atakapofika pale.” Kwa hiyo, hilo, hiyo karibu ni kweli. Kungekuwako na shimo pale.

84 Jambo pekee likupasalo kufanya ni kuchukua msimamo wako juu ya Neno la Mungu, naye Mungu atafanya njia kwa hayo mengine. Loo, msingi huo mkuu.

85 Ninaamini Yeye alisema, huku katika Luka, ninaamini ndiko, alipokuwa akishuka kutoka mlimani, Yeye aliwaambia wanafunzi, "Watu husema Mimi Mwana wa Adamu kuwa ni nani?"

Ndipo mmoja akasema, "'Yeremia,' na 'wale manabii,' na kadhalika."

Naye akasema, "Bali ninyi mwasema kwamba Mimi ni nani?"

86 Hapo ndipo Petro alipotoa lile tamshi muhimu, "Wewe ndiwe Kristo, Mwana wa Mungu aliye hai."

87 Akasema, "Heri wewe, Simoni, mwana wa Yona, kwa kuwa mwili na damu havikukufunulia hili. Bali Baba Yangu aliye Mbinguni amekufunulia hili. Na juu ya mwamba huu nitalijenga Kanisa Langu, na malango ya kuzimu hayatalishinda."

88 Ni nini basi? Juu ya ukweli uliofunuliwa wa Neno la Mungu. Kwa kuwa, "Hapo mwanzo alikuwako Neno, huyo Neno alikuwa pamoja na Mungu, naye Neno alikuwa Mungu. Naye Neno akafanyika mwili akakaa miongoni mwetu." Nalo lilifunuliwa kwa Petro ya kwamba hilo lilikuwa ni Neno la Mungu lililothibitishwa. Amina.

89 Hiyo ndiyo sababu Yeye angeweza kusema, "Ni nani anayeweza kunihukumu Mimi kwamba nina dhambi? Ni nani anayeweza kunihukumu? Kila kitu Neno limeandika juu Yangu, nimekitekeleza." Mungu alikuwa amelithibitisha, kwamba Yeye alikuwa ni Neno. Lo, hilo ndilo. Mungu alidhihirisha. Neno linasema hivyo, na kisha Mungu analifanya halisi, analitimiza, analionyesha.

90 Miaka kadhaa iliyopita, walipoliambia kanisa, "Hakuna kitu kama ubatizo wa Roho Mtakatifu, huo ni mhemko tu ambao watu walijichochea," lakini wale walioupokea, walijua huo ulikuwa ni ukweli. Walijua Mungu alikuwa halisi. Na imethibitishwa, mpaka, leo hii, mwenendo wa Kipentekoste wa Mungu kote katika mataifa, umewaleta wengi zaidi ndani ya Kristo kuliko hayo mengine yote yalivyofanya.

91 *Mgeni Wetu wa Jumapili,* sio muda mrefu uliopita, lile gazeti la Katoliki, lilisema; ninaamini ilikuwa ni mwaka kabla ya mwaka jana, ama mwaka jana, mojawapo; kwamba, "Kanisa Katoliki lilisajili tu waongofu nusu milioni. Ambapo, Wapentekoste walisajili milioni moja, na laki tano." Amina.

92 Ni kitu gani? Ni kitu kinachopanuka, Neno la Mungu, likienea kotekote. Jinsi tunavyopaswa kuwa wenye shukrani! Ni zaidi sana, hata, hata sasa Waepiskopali, Wapresbiteri, Walutheri, na wote, wanakuja kupata baadhi Yake.

Mmeona kwenye mkutano wa Wafanyabiashara, mnawasikia wakizungumza juu ya wengine: Episkopali, Lutheri, Presbiteri. Mbona, ni kwa nadra sana unasikia Mpentekoste akifanya jambo lolote tena. Hiyo ni kweli. Ni hao wengine wote. Kwa sababu gani? Wameona udhaifu wao wa kanuni zao za imani, nao wakarejea kwenye Neno. Hapo unapata msingi, kitu ambacho hakiwezi kutikiswa.

93 Unaona mle, Roho Mtakatifu akiishi Maisha Yake katika wanadamu, akijidhihirisha Mwenyewe kwa ulimwengu. Nalo linawafanya watu kumwonea Yeye kiu: Neno la Mungu lisilotikisika, lisilokanushika, lililodhihirishwa na akijionyesha Mwenyewe, Neno lenyewe likiishiwa kupitia maisha ya binadamu. Ni jambo la ajabu jinsi gani! Hakuna kitu kisicho cha hakika kuhusu hilo. Unaweza kuona mahali ambapo Mungu alifanya ahadi, na hapa inadhihirishwa. Mamia ya miaka iliyopita manabii walinena habari zake, na hapa tunaliona likitimia.

94 Kote katika ukosoaji, kote kupitia kwenye tofauti, kote kupitia kanuni za imani, jinsi wamejaribu kulikanyagia chini Neno la Mungu! Jinsi walivyojaribu kuingiza elimu badala yake. Walijaribu kuweka kibadala, kuunda dhehebu. Wamejitatanisha wenyewe. Na kutokana na hayo yote, Neno la Mungu lingali linasimama angavu na memetevu kama lilivyowahi kuwa. Ni kitu gani? Ni kitu kile kilicho hakika. Mungu alisema, "Mbingu na nchi zote zitapita, bali Neno Langu halitashindwa." Halafu, hicho ni kitu ambacho ni cha hakika. Kama unataka kujitia nanga, liweke Neno hilo moyoni mwako.

95 Daudi alisema kwamba alilificha moyoni mwake, asije akatenda dhambi. Aliandika torati Zake juu ya besera, kisha akazifunga mikononi mwake na kila mahali, akaweka Neno Lake mbele yake daima. Hiyo ndiyo njia. Weka nia yako sikuzote . . .

96 Mungu alimwambia Yoshua, "Usigeuke kulia wala kushoto, kutoka Kwake. Ndipo utakapofanikisha njia zako. Ndipo utakapositawi sana."

97 Na wakati kanisa lote litakapojiunganisha mbali na kanuni zake za imani, na juu ya Neno la Mungu, basi kanisa litasitawi sana. Hicho kitakuwa ndicho kitu ambacho kitakanyaga ukomunisti chini.

98 Ni kitu gani kilichousababisha ukomunisti . . .? Kitu hicho hicho, mnawazia "ukomunisti," wakati anapoeneza propaganda yao, na kupanuka upesi sana, kwa mamilioni, nao watu wanaogopa sana kuuhusu: kwamba ukomunisti utafifia na kufa. Hauna budi. Ukomunisti, huenda wakafanya *hili*. Huenda wakafanya *lile*. Ninaamini Mungu atautumia, lakini, hiyo ni kweli, kama tu alivyomtumia Nebkadreza. Atashambulia vikali, ma—ma—ma . . . makapi yote, ayaangamize, kwa ukomunisti.

Lakini, hilo. . . La, hayo yametosha. Lakini, angalia. Lakini kitu hicho, ukomunisti, utakuwa na mwisho wake. Ukomunisti utafikia mwisho wake.

99 Lakini Neno la Mungu halina mwisho, kwa sababu halikuwa na mwanzo. Amina. Ni la Milele pamoja na Mungu. Na ikiwa umetiwa nanga, nalo Neno limekolezwa ndani yako, wewe ni wa Milele pamoja na Neno. Amina.

100 Hauna budi kufikia mwisho wake. Vitu hivyo vyote vinatikisika. Haidhuru wanajenga nguzo kubwa jinsi gani, haina budi kuporomoka. Mambo yote yasiyo, yaliyo dhidi ya Neno hilo, ama kinyume chake, itabidi yaondoke. Itabidi yaondoke, kwa sababu Neno linakuja kwa ushindi. Hakuna kitu kinachoweza kulizuia. Mungu tayari amekwisha kusema jambo hilo.

101 Wakati Yeye anapolinena, mbingu na nchi zitapita, bali halitashindwa kamwe. Lifiche Neno hilo moyoni mwako, jinsi ya kulichukua Neno hilo na kulifanya likue. Liweke moyoni mwako, sikuzote, kwa sababu kamwe halitashindwa. Neno la Mungu halitashindwa kamwe, kwa sababu Yeye alisema halitashindwa. Kwa hiyo tunataka kuliweka juu ya hilo.

102 Sasa, Paulo alisema, katika Maandiko, kama kumfunza askari, askari kuijua sauti. Sasa, askari hana budi kujifunza sauti za ninii yake, ya buruji ama baragumu. Hajui kama baragumu imepigwa, imelia, kama a—ashambulie ama kama arudi nyuma. Iwapo hajui tofauti yake, utakuwa na jeshi lililochanganyikiwa jinsi gani? Adui hakika angepata ushindi juu ya kundi la askari ambao hawakuwa na mafunzo mazuri kuliko hayo. Amina.

103 Hiyo ndiyo shida ya makanisa yetu siku hizi. Tumewafunza kanuni za imani, zikitofautiana moja na nyingine.

104 Inatupasa kuungana. Inatupasa kuijua baragumu. "Basi hiyo baragumu ni ipi?" wanasema. Baragumu ya Injili, ndiyo Hiyo. Neno la Mungu aliye hai ndilo Baragumu. Usichanganyishe chochote na Hilo.

105 Usimwache mtu mmoja kupiga kinubi cha Kifaransa, na huyo mwingine apige buruji. Hakuna anayejua la kufanya. Inasababisha mchafuko.

106 Naye Paulo alikuwa akinena juu ya kumfunza mtu aijue sauti. Na kama tu vile sauti hiyo ilivyo, yeye anajua la kufanya hasa, kwa kuwa mpiga buruji ana amri, zitokazo kwa jemadari mkuu. Basi anapopiga baragumu hii, jeshi linajua mahali hasa pa—pa kusonga mbele hasa, na mahali pa kurudi nyuma, na kama kugeuka mkono wa kulia ama wa kushoto, ama jambo la kufanya, kwa sauti ya hiyo baragumu.

107 Sasa, jeshi, vita, daima imekuwa ni vita. Kamwe hatukujiunga na Kanisa, ama kuingia ndani ya Kanisa, tupate

kuja kwenye mandari. Lazima tutambue tunakuja kwenye uwanja wa vita.

108 Kamwe siji, ati watu wapate kunipapasa mgongoni na kusema, “Ndugu Branham, wewe ni mtu mzuri sana.” La, bwana. Ninakuja hapo nimeshika ngao. Sihitaji ngao kwa hilo. Naja na helmeti pamoja na silaha. Naja kupiga vita, kupigania kila inchi ya ardhi.

109 Mungu alimwambia Yoshua, “Kila mahali nyayo za miguu yenu zitakapokanyaga, hapo nimewapa.” Kwa hiyo, nyayo za miguu zilimaanisha umilikaji.

110 Ndipo basi kanisa linapofikia mahali, linapatana na kanuni za imani, na kupatana kwa Neno, na kupatana na ulimwengu, namaanisha, basi limeanza kushindwa. Linarudisha.

111 Tunachohitaji usiku wa leo ni askari wamiliki kila ahadi ya Kiungu ya Biblia hii, ambayo Mungu aliliahidi Kanisa, silaha zote za Mungu, na kusimama. Ndicho tunachohitaji, askari; sio kuchukua nguo rasmi za gwaride ya maonyesho ya mavazi, sikuzote ni tofauti. Wakati mtu . . .

112 Taifa lolote, tunao wapelelezi katika kila taifa. Tuna wapelelezi wa Kijerumani hapa. Tunao wapelelezi wa Kiingereza hapa. Tunao—tunao wapelelezi huko Uingereza. Wanajaribu kufanya nini? Wanajaribu kupeleleza ni nyenzo za aina gani, ni bomu la aina gani, yule mwingine alilo nalo. F.B.I. wako karibu katika kila taifa. Wanapeleleza, waone. Hivyo ndivyo wanavyoponea. Wanapeleleza waone huyo mwingine anapata bomu la aina gani. Ndipo wanakuja na kuunda lililo bora kidogo zaidi, ama wanabuni kitu cha kulikabili. Hawaaminiani, katika mataifa, maana hiyo inaonyesha ya kwamba mataifa yanatetemeka. Mbona, Uingereza ingetulipua, katika saa moja, kama tungaliwaingilia, ama sisi tungewalipua. Inahitaji tu mtu fulani kule juu anayekiongoza kitu hicho kule, anywe pombe moja ndogo ama mbili, kupita kiasi, ama akosane na kitu fulani, na ndipo hiyo inarushwa.

113 Hapa si muda mrefu uliopita, wao wangesema, kipande kidogo cha bidhaa, “Imetengenezewa Japani,” wakati wa vile vita. Wangevurumisha kitu hicho sakafuni, watembee huku na huku, kizalendo. Na sasa mtalipia gharama kubwa kwake kuliko kitu chochote mnachonunua nchini. Ni jambo gani lililotukia? Ati hilo linalipia maisha ya wavulana wale waliofia kule? La hasha.

114 Ni kitu gani? Sijali unapiga vitu vya kawaida jinsi gani, unaenda, haitamaanisha kitu. Kitatikisika. Bali kuna vita moja unavyoweza kuingia na kupata ushindi usioweza kuondolewa kwako. Hiyo ni sauti ya Injili ya Baragumu ya Neno la Mungu, na imemiliki karama na ahadi ambazo Mungu alilipa Kanisa. Hakika ndivyo. Sasa, tunaona—tunaona, kutoa sauti hii ya baragumu.

115 Sasa, kila taifa hujaribu kuwapa wavulana wao ulinzi ulio bora sana wawezao kuwa nao. Sasa, najua, wakati mwingine silaha hizi si rahisi kubeba.

116 Nilikuwa na ndugu, "Rookie," ndivyo walivyomwita, aliyeenda huko, nalo jeshi likampa kifurushi cha pauni tisini mgongoni mwake. Na hiyo ni takribani uzito wake. Wakampa sepetu, ya kuchimba shimo; bunduki, na lundo zima la makombora ya mkono. Na, loo, kamwe sijapata kuona furushi kama hilo! Maskini jamaa huyo mdogo alitembea kwa shida sana. Nao wakamshusha barabarani apate kutembea maili tano. Karibu limuue. Akasema, "Upuuzi huu wote ni wa nini? Kwa nini niihitaji maskini helmeti hii kubwa mno?" Sasa, angalieni. Jeshi linajua ataihitaji hiyo wakati mwingine. "Kwani ninataka nini na sepetu, huku kwenye barabara kuu, nikitembea?" Heri uzoee kuitumia. Huenda ukaihitaji.

117 Serikali haitatoa kitu isipokuwa ujue . . . wanajua itakubidi kukitumia. Huna budi kujizoeza kwa ajili ya hicho. Wanatafuta vitu vilivyo bora sana wawezavyo kupata, kukulinda kwavyo, kwa sababu wanavutiwa na taifa. Wanapenda ulindwe vizuri iwezekanavyo, kuziepa risasi. Hilo daima limekuwa hivyo.

118 Ilianza katika bustani ya Edeni. Naye Mungu hulifunza Kanisa Lake. Na ninii . . .

119 Mwajua, daima inatubidi kuboresha. Sasa, zile ndege za zamani tulizokuwa tukizitumia huko nyuma katika Vita vya Kwanza vya Dunia; Vita vya Pili vya Dunia, mbona, maskini vishambulizi hivyo hewani vyote vilitupiliwa mbali, walipoweka hizi ndege kubwa maalum, walizokuwa nazo. Mbona, zilikuwa ni bure. Na sasa, zile ambazo ndio kwanza watumie katika vita hivi vya mwisho, sasa zimepitwa na wakati. Hawazihitaji tena. Wanazo jeti. Na, mnaona, sikuzote mnajaribu kuboresha, kuboresha hicho kitu kwa ajili ya kujihami.

120 Lakini unajua nini? Haimbidi Mungu kuboresha. Mungu aliwapa watoto Wake, askari Wake, kitu bora zaidi walichoweza kupewa. Wakati alipowapa, Yeye aliwapa nini? Aliwapa Neno Lake katika bustani ya Edeni, naye mwanadamu alikuwa ajiimarishe nyuma ya Neno la Mungu, na hakuna ibilisi anayeweza kumpata. Dumu katika Neno.

121 Sasa, adui mpelelezi, Shetani, alijaribu kuona ni nini angaliweza kufanya ili kulivamia hilo. Kwa hiyo a—alijua hangeweza kutokea tu na kumdanganya, kwa hiyo jambo pekee angaliweza kufanya lilikuwa ni kumwingiza katika hoja. Na hilo ndilo Mungu hutumia siku hizi, kuliimarisha Kanisa Lake, ni Neno Lake. Naye Shetani hukaribia pamoja na nguvu za hoja. Shetani alijua huo ulikuwa ndio mwanya. Hapo ndipo mahali watu wangalivunjika kwa urahisi sana, ilikuwa ni kutoa hoja.

122 Unasema, "Sasa, hebu tu nihojiane nawe. Sasa kuna haja?"

123 Kama Mungu alisema lilihitajika, linahitajika, kama itatubidi kulia, na buuhuu, na kufanya yote *haya*. Kama Mungu alisema kwamba ubatizo wa Roho Mtakatifu ni muhimu, Sijali ni mzito kiasi gani, na kiasi gani cha ulimwengu kinachokubidi kuachilia, itakubidi kuutumia, moja ya siku hizi, upate kuishi. Ndio njia ya pekee ya kuponea.

124 "Sasa, hivi inatupasa kufanya uponyaji wa Kiungu, wakati tukiwa na madaktari walio bora sana ulimwenguni?"

125 Mungu aliwapa uponyaji wa Kiungu maana alijua itawabidi kuutumia. Aliwapa karama za Roho.

126 Na mara Shetani alipomkaribia Hawa, alianza kuhojiana naye. Sasa, "Hakika, hakika, Mungu asingeweza kufanya *hilo*."

127 Watu husema siku hizi, "Hakuna kitu kama kuzimu." Wengi sana wao hukwambia hivyo. Mnaona? "Loo, hakika Mungu asingeweza kuwachoma moto watoto Wake."

128 Bila shaka, Yeye hawachomi moto watoto Wake. Bali ibilisi atawachoma, wake. Wewe ni mtoto wa nani? Hilo ndilo jambo linalofuata. Kuzimu kuliumbiwa ibilisi na watoto wake, sio watoto wa Mungu. Hakuna mmoja wao atakayeenda huko. Hiyo ni kweli. Inategemea wewe ni mtoto wa nani.

129 Sasa, Mungu alimpa Hawa na Adamu Neno Lake, wala kamwe hajalibadilisha. Daima amekuwa na . . . Mkristo, ama mwaminio, Kinga yake ni Neno.

130 Mbingu na nchi zitapita. Kila kanuni ya imani itapita. Kila dhehebu litaanguka. Kila taifa litazama. Lakini Neno la Mungu litasimama, Milele. Kutakuwako na wakati ambapo nyota ya asubuhi haitaangaza tena. Kutakuwako na wakati ambapo jua halitaangaza, nao mwezi hautaangaza, wala ulimwengu hautazunguka katika mzingo wake.

131 Lakini Neno la Mungu daima litadumu vile vile. Naam. Hilo ni kitu kisichoweza kusogezwa, kitu ambacho unaweza kukitegemea. Ni la hakika. Mungu akisema chochote, hakika kitatukia.

132 Kama Yeye alisema, katika bustani ya Edeni, kwa ajili ya Mkombozi, Yeye angemtuma Masihi, lilikuwa hakika litatukia. Ingawa miaka elfu nne walingoja, bali Yeye aliwasili. Ilibidi aje kwa sababu ilikuwa ni Neno la Mungu lililoahidiwa.

133 Mungu aliahidi kumtuma tena. Atawasili. Sijali ni makafiri wangapi na wenye kushuku watakaoinuka, chochote wafanyacho, jinsi ukomunisti unavyoenea, Yesu Kristo atakuja, na atajipatia Kanisa ambalo limeoshwa kwa Damu, na kulipeleka kwenye safari ya angani kwenda Mbinguni. Kwa nini? Hakika litatukia. Neno la Mungu lilisema hivyo.

134 "Kama unaweza kuamini, mambo yote yanawezekana." Hilo ni hakika. Mungu alisema hivyo, nalo haliwezi kusonga, haliwezi

kutikiswa. Mungu alisema hivyo, kama tu utadumu pamoja nalo (Sasa . . .) na kuwa na imani nalo, kulisadiki.

135 Siyo sauti isiyojulikana. Mungu hawezi kutoa sauti isiyojulikana. Kanuni za imani zinaweza kutoa sauti isiyojulikana. Madhehebu yanaweza kuhubiri sauti isiyojulikana. Bali Mungu hawezi kutamka sauti isiyojulikana. Nalo hili Neno ni Mungu. Wala hakuna kutoeleweka kulihusu. Linaeleweka kwa kila hali.

136 Sasa, lile Kanisa kuu limevikwa silaha kwa Neno. Sasa, wakati Yesu alipokuja, Yeye alitumia silaha ile ile? Hakika aliitumia.

137 Shetani alipomjia, katika nguvu zake zote, naye akasema, "Kama wewe ni Mwana wa Mungu, fanya mambo *fulani, fulani*."

138 Yeye alisema, "Imeandikwa . . ." Moja kwa moja kurudi kwenye Neno. Shetani akamjaribu vikali zaidi kidogo. Lakini, Yesu, akarudi moja kwa moja pamoja na Neno, "Imeandikwa . . ."

139 Hapo Yeye alibakia, juu ya Neno hilo, akituonyesha kama mfano. Kama Yeye alivyosema katika Wakorintho wa Kwanza, wa kwanza . . . Yohana Mtakatifu 14:13, "Nimewapa mfano." Nao huo ni mfano, kwamba inatupasa kusisitiza, inatupasa kuweka matumaini yetu kikamilifu katika Neno la Mungu. Kingine chochote na kiwe ni uongo. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

140 Hicho ni kitu kimoja kilicho cha hakika. Mungu alifanya ahadi. Mungu ataitimiza hiyo ahadi. Wao wanasema, "Jambo *hili* linawezaje kutukia? Yeye anawezaje kulikusanya kundi la watu, pamoja na neema ya Kunyakuliwa, wapate kupaa juu?" Sijui jinsi atakavyolifanya. Sio kazi yangu kuuliza jinsi atakavyolifanya. Ni jukumu langu kuwa tayari tu kwa ajili yake. Yeye aliliahidi. Litatukia. Aliliimarisha Kanisa Lake kwa Neno.

141 Basi jambo la kwanza lilikuwa ni hoja. Sasa wao wanasema, "Hivi si ni wazi sasa, kama nikiwa mfuasi wa kanisa *hili*, hivi hilo si ni zuri tu kama kanisa *lile*?"

142 Kunalo Kanisa moja tu unaloweza kuwa mshiriki wake. Kamwe hutaweza kujiunga na Hilo. Huenda ukajiunga na chama, chama cha Methodisti, na chama cha Presbiteri, na chama cha Baptisti, na chama cha Kipentekoste. Bali unazaliwa katika Kanisa la Yesu Kristo, kwa hiyo hilo hapo Kanisa.

143 Hayo ni vyama, ambapo watu hukusanyika pamoja, kama kunguru kuketi kwenye tawi *hili*, na hua kwenye tawi *hili*, na—na kadhalika. Huo ni ushirika wenu mlio nao pamoja, wakati mnaposhiriki mlo ule ule.

144 Lakini inapofikia Kanisa la Yesu Kristo, kuna njia moja peke yake. Hiyo ni Kuzaliwa. Kuzaliwa!

145 Ni kama tu mtu, kama vile nimesema mara nyingi, kama ndege mweusi aliyeketi kwenye tawi, akijaribu kuchomelea manyoya ya tausi kwenye mabawa yake, na kusema, "Mnaona, mimi ni tausi mwenye hatua za mikogo." Mnaona? Yeye alijichomelea hayo manyoya, yeye mwenyewe. Kama alikuwa ni tausi halisi, asili yake ingekuza unyoya wa aina hiyo.

146 Iwapo Kanisa la Mungu aliye hai ni Kanisa la Mungu aliye hai, litazaa Neno la Mungu aliye hai. Haikubidi kuongezea manyoya ya tausi popote. Na kila unyoya mle utakuwa umeunganishwa na tausi. Unaweza kuamini hilo. Na kila unyoya uliounganishwa kwenye Kanisa la Mungu utakuwa ni Neno la Mungu. Yeye kamwe hataingiza chochote kingine ila Neno. Amina. Maana, asili ya Roho huzaa tu Neno. Amina. Ninaanza kujisikia kubarikiwa. Kweli.

147 Si jambo lolote unalojaribu kufanya, si kitu unachojitengenezea. Huwezi kujitengenezea di-. . .Huwezi kujitengenezea wokovu. Huwezi kujitengenezea karama. Huna budi kuzaa karama. Bila shaka. Mnaona? Ko—kondoo hatengenezi, hatengenezi sufi. Yeye yuna sufi kwa sababu yeye ni kondoo. Yeye huzaa tu sufi. M—m—mcheri hautengenezi cheri. Huzaa tu cheri, kwa sababu uhai wake uko hivyo.

148 Nalo Kanisa la Mungu aliye hai haliliingizi Hili, kujaribu kujifanya lionekane kama kitu fulani. Wao tayari wako jinsi walivyo, kwa neema ya Mungu. Nalo Neno la Mungu limeunganishwa nao, nao wameunganishwa na Neno. Nazo kazi zilizotolewa katika yule mkamilifu, Yesu Kristo, Mungu aliyedhihirishwa katika mwili, zitajizalisha kupitia kwa kila mwaminio aliyezaliwa mara ya pili. Yeye alisema hivyo. Amina. Hakuna lingine. Sasa, hicho ni kitu cha hakika.

149 Sasa, ingekuwa kidogo—kidogo inatatanisha kwa mtu, kama kamwe hakujua sauti halisi ya baragumu. Sasa, mtu ambaye kamwe hajafunzwa kuijua baragumu, wala kamwe hajaisikia, vema, huenda akachanganyikiwa kidogo anaposikia kitu fulani kikitoa sauti tofauti na ile aliyoisikia. Sikuzote amesikia, "Jiunge na kanisa. Peleka barua yako *hapa* na *hapa*." Huenda hilo likawa ni sawa. Hilo tu ndilo ajualo.

150 Lakini unapofikia kurudi, kuhusu ubatizo wa Roho Mtakatifu, kunena kuhusu nguvu za Mungu na mambo afanyayo Yeye; na jinsi inavyowafanya wanawake na wanaume, wote, kujitakasa, kutokana na maisha ya dhambi; jinsi inavyowafanya kutembea kitauwa, kiaminifu. Na mambo lifanyayo, na kuleta ubatizo, kunena kwa lugha, kuwaponya wagonjwa, kuwatoa pepo, kutabiri, karama, loo, maono, kila kitu Kanisani. Haleluya! Hiyo ni kweli. Linapofanya hivyo, basi kidogo huwatatanisha hao ambao kamwe hawajasikia baragumu ya aina hiyo.

151 "Vema," unasema, "kanisa langu halifundishi hayo." Basi haliipigi baragumu ya Injili. Utukufu! Kweli.

152 Bali kwa askari hao waliofunzwa, haleluya, wanapoisikia sauti ya baragumu hiyo, wanajua jinsi ya kusimama kwa utaratibu. Twendeni, askari Wakristo! Utukufu! Loo, hiyo ni hakika!

"Unajuaje ni hakika?"

Iko kwenye Neno.

"Vema," unasema, "kanisa letu halifundishi Hayo."

153 Lakini baragumu inalinena. Sitaki kufunzwa kufuata kanuni ya imani ya kanisa, maana itatikisika na kuanguka. Bali kama umefunzwa kwenye Neno, mbingu na nchi zitapita, nalo Neno hili halitapita kamwe. Kila kanuni ya imani, kila kitu kingine, kitaanguka. Bali Neno hili halitashindwa kamwe. Amina. Hiyo ndiyo sauti. Hiyo ndiyo sauti ninayotaka kusikia. Naam, bwana.

"Loo," unasema, "nitajuaje?"

154 Yesu alisema, "Kondoo wangu huisikia sauti Yangu. Wanaijua baragumu Yangu." Yeye alisema, katika Yohana Mtakatifu, mlango wa 14 na kifungu cha 12, "Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo Mimi yeye naye atazifanya." Sasa, Yeye alisema hivyo.

Kama mtu akisema, "Vema?"

155 Waebrania 13:8 ilisema, "Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele."

"Loo," wao wanasema, "kwa njia fulani."

156 Sasa, kondoo halisi atasema, "A-ha. Loo, kitu fulani kilitoa sauti kali, katika hilo. Hilo halisikiki kuwa sawa. Loo, hapana budi kilikuwa ni chombo cha pembe ya Kifaransa. Hiyo haikuwa ni baragumu, maana Biblia haitoi sauti yoyote isiyoeleweka."

157 Inasema, "Mtapokea Roho Mtakatifu." Sio, "Huenda mkapokea." "Mtapokea, kila mmoja." Kwa muda gani? "Kwa watoto wenu, na kwa watoto wa watoto wenu, na wale walio mbali, hata kwa wote watakaoitwa na Bwana Mungu wetu wamjie." Itatoa sauti ya baragumu katika kila jamii na kila kizazi, nao wataisikia sauti Yake. Wataiamini, wale waliokusudiwa Uzima. Amina. Wataiamini kwa sababu wanajua ni baragumu ya Injili ikilia. Si isiyojulikana. Kila askari anajua jinsi ya kusimama.

158 Sasa, mliwaona Petro, na Yohana, Yakobo, na kanisa la mwanzoni, wakipiga hatua kuelekea huku, kwa sababu ile baragumu, Yesu, alisema, "Enendeni ulimwenguni kote, mkaihubiri Injili." Marko 16, mnaona, "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio." Tunamwona Petro, Yakobo, Yohana, na hao wengine wakijipanga, wakienda taratibu kwenye Hilo.

159 Ati nasi tugeuke upande mwingine, kutoka kwa Hilo? Mmoja akisonga mbele, mwingine akirudi nyuma? Mmoja akisema, "Vema, hiyo ilikuwa ni kwa ajili ya mwingine. Hiyo, hiyo—hiyo sauti, ilikuwa kwa ajili ya mwingine." Loo, la. Haiwezi kuwa hivyo.

160 Jeshi lote la Kikristo huisikia baragumu. Mungu alisema hiyo ilikuwa ndiyo baragumu. Hawezi kuibadilisha. Hiyo ndiyo sauti ambayo Yeye alisema ingetolewa. "Hivi watu wote watajua," nalo Kanisa linaondoka.

161 Baadhi yao hawaamini katika Kuja Kwake kimwili. Biblia ilisema Yeye atakuja, kwa hiyo tunakutazamia Kuja Kwake. Ikiwa Yeye hayupo hapa usiku wa leo, tutamtazamia asubuhi. Kama hayupo hapa asubuhi, tutamtarajia kesho usiku. Nasi tutaendelea kutazamia. Kama tukilala usingizi, ninii yetu—yetu. . .hatujachoka bure. "Kwa kuwa baragumu ya Mungu itatoa sauti hiyo ya mwisho, nao waliokufa katika Kristo watafufuka. Nasi tulio hai na tuliosalia tutanyakuliwa pamoja nao, kumlaki Bwana hewani, na milele tuwe huko." Hiyo ndiyo sauti ya baragumu. Niishi ama nife, haileti tofauti yoyote. Nitaisikia hiyo sauti. Nitafufuka. Utukufu kwa Mungu! Fufuka. Loo, naam. Naam.

162 Yesu alisema, ya kwamba, "Kondoo Wangu huisikia sauti Yangu." Yeye alikuwa Neno lililodhihirishwa. Wakati ninii. . . Hivyo ndivyo kondoo Wake wanavyomjua.

163 Sasa waangalieni wale Mafarisayo na hao kwenye siku hiyo. "Loo," wao walisema, "Mtu huyu ni Beelizebuli." Wakati alipomwambia yule mwanamke kisimani, ambapo, kuhusu dhambi zake, waume zake aliokuwa nao, wakati alipomwambia Nathanaeli mahali alipokuwa, chini ya mti mahali Filipo alipomwita, chini ya mtini, akiomba, mbona, hao walimu wa siku hiyo walisema, "Mtu huyu ni Beelizebuli. Yeye ni ibilisi. Yeye ni mpiga ramli."

164 Bali hiyo haikuwa hivyo kwa Petro, Yakobo, na Yohana, hao wengine. Wao walilijua. Kwa nini? Walijua ya kwamba Mungu alisema kwamba Masihi atakapokuja, chini ya sauti iliyovuviwa ya Musa, Yeye atakuwa ni nabii. Basi walipoyaona mambo hayo aliyosema yakidhihirishwa na kufanywa makamilifu, walijua hicho kilikuwa ni chakula cha kondoo. Walijua hiyo ilikuwa ni baragumu. Nao wakaanza kuifuata. "Kondoo Wangu wanaijua," maana waliliona Neno la Mungu likidhihirishwa.

165 Sasa, watu siku hizi, hawaamini kuna kitu kama ubatizo wa Roho Mtakatifu. Wanashuka huku ama mahali pengine ambapo wanaye Roho Mtakatifu, nao wanaiona ahadi ya Mungu ikitimizwa kikamilifu, mbona, "Kondo Wangu huisikia sauti Yangu." Wanajua sauti ya baragumu hiyo kwa maana ni Biblia. "Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele." Yeye angali ni Waebrania 13:8, kabisa.

166 Sijali, sasa, haileti tofauti hata kidogo ni vyombo vingapi mbalimbali vya pembe vya kanisa vinalia. Tuna pembe nyingi sana za kanisa, mwajua, zikilia kila kitu huku na huku, zikisema, "Loo, siku za miujiza zimepita. Hakuna kitu kama uponyaji wa Kiungu."

167 Loo, kondoo halisi hawasikilizi hayo. Lakini wao wanaisikiliza ile baragumu, ile ya kweli.

168 Pembe hiyo ya kanisa huenda ikatoa sauti yoyote. Huenda wewe. . . Angalieni kile zilicho nacho siku hizi, hizo pembe za kanisa. Moja inakimbia *huku*, na nyingine inakimbia *kule*. Naye ibilisi ameketi kitako, akisema, "Jamani, wanashambuliana tu. Hivyo tu. Hata hainibidi kuunyosha mkono wangu."

169 Lakini, ndugu, hebu wote wavae silaha wakati mmoja, warudi kwenye utaratibu wa kawaida. Loo, jamani! Ndipo utaona "twendeni, askari Wakristo," kweli, pasipo kuzisikiliza pembe fulani, bali kuisikiliza baragumu.

170 Hebu tusimame tu, kwa dakika moja, na kurudi nyuma na kuwaangalia wachache sasa. Tunakaribia kufunga, maana sitaki kuwaweka hapa kwa muda mrefu sana. Lakini hebu turejee nyuma na kuangalia baadhi ya wale walioisikia sauti hii. Hebu tuchukue. . . Nao walikuwa na hakika. Sasa, nimewaonyesha kila kitu kingine hakijulikani. Hebu tumchukue tu mzee mmoja, kwa muda kidogo.

171 Hebu tumchukue nabii Ayubu. Sasa, mtu huyo alipitia majaribu, bali alijua ya kwamba Mungu alihitaji sadaka ya kuteketezwa. Hiyo ndiyo Mungu aliyohitaji, na hiyo tu ndiyo aliyohitaji. Na haidhuru ni maafa mangapi yaliyotokea nyumbani mwake. . . Mungu daima haninii. . .

172 Unapoona lolote likienda kombo kwa jamaa fulani, hilo halimaanishi kwamba anacharazwa na Mungu. Huenda isiwe kwamba yuko nje ya mapenzi ya Mungu. Yeye anajua moyoni mwake kama anaisikiliza baragumu ama la.

173 Mungu alihitaji dhabihu hii ya kuteketezwa, naye Ayubu akasimama moja kwa moja juu yake. Hivyo tu. Wao walisema, "Ayubu, wewe ni mtenda dhambi kisiri. Unafanya makosa fulani." Lakini yeye alijua vizuri zaidi. Alidumu papo hapo, kwa sababu alikuwa ameisikia sauti ya baragumu, naye akadumu nayo papo hapo.

174 Ndipo, hatimaye, kwenye mwisho kabisa, wakati alipokuwa. . . Ibilisi alikuwa ameachiliwa juu yake, na akaichukua familia yake, kisha akawachukua watoto wake, akawachukua ngamia wake, na kuchukua mali yake yote, akaiharibu afya yake. Akaketi kwenye lundo la majivu. Ilionekana kana kwamba kila kitu kilikuwa kimekwisha. Lakini angali alisema, "Ninajua Mkombozi wangu yu hai. Siku za mwisho atasimama juu ya nchi. Ingawa mabuu ya ngozi yanauharibu mwili huu, hata hivyo katika mwili wangu

nitamwona Mungu." Hakuna kitu kisicho cha hakika kuhusu hilo, sivyo? Sio, "Kwa namna fulani na—na—na—nafikiri Yeye yu hai." Yeye alisema, "Najua Yeye yu hai, na Yeye atasimama katika siku za mwisho juu ya nchi. Ingawa mabuu ya ngozi yanauharibu mwili huu, hata hivyo katika mwili wangu nitamwona Mungu." Loo, jamani! Lilitukia. Alikuwa na uhakika kabisa.

175 Ibrahimu, akitembea kondeni siku moja, alimsikia Mungu akisema, "Ibrahimu, Mimi ninaenda . . . " Alikutana na Ibrahimu kabla ya Neno lililoandikwa, ndipo Yeye akasema, "Ibrahimu, nitakupa mwana kwa mke wako, Sara." Naye alikuwa na umri wa miaka sitini na mitano wakati huo, naye Ibrahimu alikuwa na sabini na mitano. Nao wakajiandaa kwa ajili yake, wala hakuona aibu kushuhudia. Alijua atampata huyo mwana.

176 Nayo Biblia ilisema, "Hakusita katika ahadi ya Mungu kwa kutokuamini, bali alishawishika kabisa." Amina. Alishawishika kabisa, hiyo inamaanisha ya kwamba amekutana na yakini. Amina. Jambo ndilo hilo. Yakini ndio mwisho wa safari. Ndilo jambo la mwisho. Ni—ni yote.

Yeye alisema, "Nimeshawishika kabisa ya kwamba, yale Mungu aliyoahidi, Mungu anaweza kutimiza."

177 Hivi wewe, usiku wa leo, umeshawishika kabisa ya kwamba huyu ni Roho Mtakatifu? Hivi umeshawishika kabisa, hii ndiyo njia? Umeshawishika kabisa, Yeye ni Mponyaji? Hivi umeshawishika kabisa ya kwamba Yeye yuaja tena? Hivi umeshawishika kabisa Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Amina. Kushawishika kabisa! Naam.

178 Hebu na tumchukue mwingine, Eliya, akisimama pale juu ya mlima. Alikuwa amebishana na Yezebeli na uso wake uliopakwa rangi, na kidogo alikuwa akichoshwa nao. Karibu wanawake wote wanajifananisha na mama taifa, labda nywele mkato wa kichwa-maji na chochote walichokuwa nacho katika siku hiyo. Yeye alikuwa amelibishania hilo sana hata lilikuwa karibu li—limemwangamiza.

179 Moja kwa moja, Mungu akamwambia, "Shuka uende kule. Unajua, inanyesha karibu kila siku mbili ama tatu kwa juma, huku. Bali wewe mkabili Ahabu, ukamwambie, 'BWANA ASEMA HIVI. Umande hautaanguka kutoka mbinguni mpaka nitakapouagiza.'" Loo, jamani!

180 Yeye hakusema, "Sasa, Ahabu, labda, huenda ikawa itatendeka hivi." Loo, la. Yeye alishawishika kabisa, hakuna kitu kisicho hakika. "Umande hautaanguka, mvua haitakuja, mpaka nitakapoiagiza." Amina. Utukufu! Loo, kwa nini? Yeye aliisikia baragumu. Ilikuwa inaeleweka. Yeye alimjua Mungu wake. Alijua jambo fulani. Wakati Mungu aliponena neno hilo,

mbingu zote na nchi zitapita mpaka li—litendeke. Ingebidi litendeke. Yeye alishawishika kabisa.

181 Sasa, Yeye alisema, "Eliya, ninakutaka upande uende kule katika mahali palipo pakavu kuliko pote nchini, moja kwa moja mlimani ambako hamna chemchemi. Bali ninayo moja kule kwa ajili yako."

182 Yeye alishawishika kabisa. Alipanda juu ya mlima akaketi chini karibu na kijito cha Kerithi. "Na sasa ninaenda kufanya nini hapa juu?"

"Tayari nimewaamuru kunguru wakulishe."

183 "Sasa, ni vipi hao kunguru . . . Sasa, ngoja kidogo, Bwana"? La, la. Baragumu ililia. Hilo latosha. "Litatukiaje? Sijui. Sijali. Mnaona? Siyo kazi yangu kujisumbua juu ya hilo. Hiyo ni kazi ya Mungu. Yeye alisema aliwaamuru kunguru."

184 "Vema, Bwana, naomba unielezee, na uniambie tu ni wapi hao . . . hao kunguru walienda kwenye shule gani kule, kujifunza kuzungumza Kiebrania? Ni ninii ya jinsi gani . . . Wanapika kwa stovu za gesi, ama wana moto wa kuni, ama wanafanyaje hilo? Nao ni wapi watakaponinii . . . Watamchinja mnyama wa namna gani? Hao ni ndege mdogo tu. Watanichinjiaje mnyama, wapate kuniletea sambusa ya nyama?" Mnaona? Mnaona? Hilo halikuulizwa.

185 Mungu, pa—parapanda ya Mungu, sauti yake ilitoa sauti na kusema, "Nimefanya!" Sio, "Eliya, huenda nikalifanya." "Nimelifanya. Nitalifanya. Nimelifanya tayari." Amina.

186 Huyo ni Mungu wetu, usiku wa leo. Sio, "Yeye atalifanya." Tayari amelifanya. Amina. Tayari amelifanya. Amina. Sio, "Atalifanya; huenda akalifanya; labda atalifanya." Amelifanya tayari. "Nimewaamuru kunguru."

187 Yeye alimtoa Roho Wake kwa watu wote. Alizitoa baraka Zake. Alipaa Juu, akawapa wanadamu vipawa. Mtu fulani atalipata. Mtu fulani atalikataa. Siyo kazi yangu jinsi linavyokuja. Ni kusudi tu lifike pale. Mungu alisema lingekuwa hivyo, na ndivyo lilivyo. Petro alisema, kwenye Siku ya Pentekoste, "Tubuni, kila mmoja wenu, mkabatizwe, Jina la Yesu Kristo kwa ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtapokea kipawa, Roho Mtakatifu." Atakujaje? Sijui mimi. "A—ahadi hii ni kwa ajili ya watoto wenu, kwa wale walio mbali, hata wote watakaoitwa na Bwana Mungu wetu wamjie." Sasa, usingeweza kuelezea hilo vinginevyo. Parapanda imelia tayari, nami ninaiamini. Niliitii, na nikaipata. Amina. Sasa hebu jaribu kunibishia niliache hilo wakati mmoja. Amina. Loo, mimi si mkamilifu. La.

188 Kama usiku ule, maskini yule dada mweusi, yeye alisema, "Mzee, naweza kutoa ushuhuda?"

"Naam, mama."

189 Akasema, "Ninataka kusema jambo hili moja." Akasema, "Mimi—mimi—mimi haiko jinsi ninavyotaka kuwa." Kisha akasema, "Mimi haiko jinsi ninavyopaswa kuwa. Lakini, kuna jambo moja nijualo, mimi haiko vile nilivyokuwa."

190 Kwa hiyo, hilo, hivyo ndivyo tunavyojisikia kuhusu hilo sasa. Siko jinsi nilivyokuwa, kwa sababu nimeokolewa usiku wa leo, kwa neema ya Mungu, na kuupokea ubatizo wa Roho Mtakatifu, juu ya lile agizo. Ilimwagwa huko nje kwenye Siku ya Pentekoste, ile ahadi ilitolewa, nami nikaiamini. Hakuna kitu kisicho cha hakika. Niliisikia sauti. Nikaitii, nami nina hakika hivyo ndivyo ilivyo. Bila shaka. Ninajua ndivyo ilivyo. Hakika.

191 Simeoni, yule mtakatifu mzee mwenye umri wa kadiri miaka themanini, mamia ya miaka tangu nabii hata kuwa duniani, bali akitembea huku na huku akiwa na sifa kuu. Roho Mtakatifu alizungumza naye siku moja, kasema, "Simeoni, unajua, hutaona mauti mpaka utakapouona wokovu wa Bwana." Utukufu!

192 Labda kuhani mkuu, akizipangusa ndevu zake mara chache, na kusema, "Simeoni, inakupasa kuzichanua ndevu zako upande huo mwingine."

Akasema, "Hiyo haileti tofauti yoyote."

"Unajuaje uko sahihi?"

"Roho Mtakatifu aliniambia hivyo. Sitaona mauti."

193 "Mbona, Simeoni, mbona, wewe ni . . . Mbona, uko tayari kufa sasa hivi."

194 "Loo, sijali usemayo. Lakini Mungu aliniambia ya kwamba sitaona mauti mpaka nitakapouona wokovu Wake. Hakuna chochote kisichojulikana. Sitakufa. Siwezi kuona mauti mpaka nitakapomwona." Amina. Jambo ndilo hilo.

"Utafanyaje jambo hilo, Simeoni?"

"Mimi, hiyo si kazi yangu."

"Yuko wapi, Simeoni?"

"Sijui."

"Unajuaje utamwona?"

195 "Mungu alisema hivyo. Jambo ndilo hilo. Ni Neno. Sitaona mauti mpaka nitakapomwona." Loo, jamani!

196 "Loo, maskini jamaa mzee. Hakika, amerukwa na akili, mwajua. Kwa hiyo achaneni tu naye."

197 Lakini yeye alimwona, hata hivyo. Naam, bwana. Mungu hufanya njia kwa ajili ya watu hao watakaoliamini Neno Lake.

198 Yesu, alipokuwa hapa duniani, naye alikuwa amesimama pale kwenye kaburi la Lazaro.

199 Ama, kabla ya hapo, wakati alipokuwa akihojiana na—na hao watu, wakinena juu ya vile Yeye, akiwa bado hajapata umri

wa miaka hamsini, naye alisema amemwona Ibrahimu. Mnaona jinsi alivyokuwa na hakika? Alisema, "Ibrahimu asijakuwako, MIMI NIKO. MIMI NIKO." Sio, "Nilikuwa, ama nitakuwa." Bali, "MIMI NIKO. Nina hakika."

200 Kisha, Yeye akasema, kwenye kaburi la Lazaro, kabla hajashuka kule, Yeye alisema, alimwambia Martha, Akasema, "Mimi ndimi ufufuo, Uzima." Sio, "Ninapaswa kuwa, ama nitakuwa." Lakini, "MIMI NIKO." Amina.

201 "Ndugu yangu, kama ungalikuwa hapa, asingalikufa. Lakini hata sasa, Bwana, lolote utakalomwomba Mungu, Mungu atakupa."

Yeye akasema, "Ndugu yako atafufuka tena."

202 "Loo, atafufuka katika siku za mwisho, kwenye ufufuo wa kiama. Alikuwa ni mvulana mzuri. Naam, ninaamini atafufuka."

203 Bali Yesu akajinyosha kidogo, mwenyewe, juu, kasema, "Lakini Mimi ndimi ufufuo na Uzima." Sio, "Nitakuwa; ninapaswa kuwa," ama kadhalika. "MIMI NIKO." Hakuna kitu hapo, hakuna cha kusitasita, kutikisika juu ya hilo. Hakuna kisichoeleweka. Kilikuwa ni cha kweli.

204 "Mimi ndimi ufufuo na Uzima. Yeye aniaminiye Mimi, ajapokufa, atakuwa anaishi. Kila aishiye na kuniamini Mimi hatakufa kamwe." Sasa, sio, "Huenda wasife; labda hawatakufa." "Hawatakufa." Hakuna kitu, hakuna kisicho hakika kulihusu. Hawatakufa.

205 "Yeye ayasikiaye Maneno Yangu na kumwamini Yeye aliyenipeleka yuna Uzima usio na mwisho, wala hata hataingia Hukumuni, bali tayari amepita kutoka mautini kuingia Uzimani."

206 "Ati haiwapasi kuingia Hukumuni"? Hawataingia Hukumuni. Amina. Yeye aliichukua Hukumu yangu. Sina shughuli yoyote kule. Amina. Haya basi. "Nimepita kutoka mautini kuingia Uzimani." Loo!

207 Sasa yeye alisema aliliamini. Sasa, Yesu kamwe hakusema, "Vema, unajua, kwa kuwa unaamini hilo, nawe unajua kwamba mimi ni Neno, na—na mimi—mimi . . . Unajua kwamba Mimi ndiye aliyekuwa aje. Umekiri hilo. Unaliamini. Nitakwambia kile huenda tukafanya. Hebu twende tukawakusanye wazee, na tushuke twende tuone kama tunaweza kufanya lolote kulihusu." La, la. Yeye alisema, "Nitaninii . . . " Sio, "tushuke tuende *nione* kama ninaweza kumfufua." "Nitaenda nikamwamshe." Amina. Sio, "Nita—nitajaribu." "Nitamwamsha." Hakuna chochote kisicho hakika. Hiyo haikuwa sauti isiyojulikana, hapo aliposema, "Nitamwamsha. Nitamwamsha."

208 Na yuyo Huyo alisema, "Nitafanya," nilikutolea ahadi. Haleluya! Loo, jamani! Amina.

"Nitaenda nikamwamshe."

209 Tena Yeye akasema, "Liharibuni hekalu hili, nami nitaona kile ninachoweza kufanya kulihusu"? "Liharibuni hekalu hili, nami nitalisimamisha tena katika siku tatu." Hakuna kisicho hakika. "Sasa nitajaribu. Ninyi nyote huenda mkasimama hapo mwone kama ninaweza kufanya hivyo ama siwezi"? Aa, la. "Nitalisimamisha." Hakuna kisicho hakika. "Nitalisimamisha. Ni—ninyi liharibuni; nitalisimamisha." Loo, jamani!

210 Kwa nini? Alijua ya kwamba Yeye alikuwa Mtu huyo, katika Maandiko, ambaye Daudi alinena habari zake. "Sitaiacha nafsi Yake kuzimuni, wala sitamwacha Mtakatifu Wangu aone uharibifu." Naye alijua alikuwa amehesabiwa katika ahadi hiyo ya Maandiko, kwa hiyo basi Yeye alikuwa na hakika.

211 Sasa, hivi hatuwezi kuwa na hakika hivyo? Tunamchukua Yeye, mfano, kwa ajili ya mambo mengine. Mradi tu Neno la Mungu lililisema, hivi hatuwezi kuwa na uhakika kuhusu Neno kama Yeye alivyokuwa nao kulihusu?

212 "Mimi ndimi ufufuo na Uzima." "Nitalisimamisha tena." Amina. Kwa nini? Yeye alijua Neno lilinena kulihusu, na Yeye alikuwa na hakika ya kufufuka.

213 Kama mimi ndimi mtu yule pale katika Yohana 5:24, "Yeye alisikiaye Neno Langu na kumwamini Yeye aliyenipeleka, yuna Uzima wa milele, nami nitamfufua tena katika siku za mwisho. Hataingia Hukumuni; amepita kutoka mautini kuingia Uzimani." Hao ni—hao ni sisi. Basi tunahofia nini? Kuna shida gani?

214 Inaleta tofauti gani umevaa chapa gani? Unajiita *hiki, kile,* ama *kinginecho*. Sisi ni watoto wa Mungu, kwa neema ya Mungu. Tumejazwa na Roho Mtakatifu, kwa neema ya Mungu. Inaleta tofauti gani kuhusu kama *huyu* ni *kile* ama *kile*, kama yeye ni Mpresbiteri, Mmethodisti, Mbaptisti? Kama yeye amejazwa na Roho Mtakatifu, yeye anao Uzima ufufuao ndani yake. Amina. Naam. Sasa, kwenye Siku ya Pentekoste . . .

215 Yesu aliwaambia, katika Luka 24:49, "Tazama, ninatuma ahadi." Sio, "Huenda nikafanya hivyo. Nitaona kile ninachoweza kufanya kulihusu." "Nitatuma ahadi ya Baba Yangu juu yenu. Lakini nendeni kule kwenye mji wa Yerusalemu na kungoja mpaka mtakapovikwa nguvu."

216 Sasa, vipi kama wangengoja, tuseme, loo, siku sita, waseme, "Kwani tunangoja nini? Ninaamini tunapaswa kuikubali kwa imani. Sivyo?"

217 Vipi kama Yakobo alisema, kwenye—kwenye siku ya tisa, kasema, "Simoni, njoo hapa kwa dakika moja. Unajua, hivi majuzi nilikuwa na namna fulani ya hisi ya kigeni. Unaona? Na unajua ninaloamini? Na—na—naamini Yeye hatutaki sisi kungojea tu hapa. Ninaamini ta—tayari tumeipata. Hivi hufikiri

hivyo? Hebu tuendelee na kazi yetu. Hebu tuendelee na huduma yetu"? Loo, kamwe isingalitendeka.

218 Kwa nini? Walijua ya kwamba nabii alisema. Sasa sikilizeni. Nabii alisema, "Amri lazima iwe juu ya amri, kanuni lazima iwe juu ya kanuni, juu ya kanuni; hapa kidogo na pale kidogo." "Shikilia yaliyo mema." "Kwa kuwa kwa midomo ya watu wageni, na kwa lugha nyingine nitasema na watu hawa. Na hii ndiyo raha, sabato." Walijua jambo fulani lilikuwa litukie wakati ilipokuja.

219 "Nitaimwaga Roho Yangu katika siku ya mwisho." Yoeli 2:28, "Itakuwa katika siku za mwisho, asema Mungu, nitaimwaga Roho Yangu juu ya wote wenye mwili, na wana wenu na binti zenu watatabiri. Juu ya wajakazi wangu na watumishi wanawake nitaimwaga Roho Yangu, katika siku hiyo. Nitaonyesha ishara mbinguni juu na—na katika nchi chini, na moto, na moshi, na mvuke."

220 Walijua ya kwamba ilibidi kuwe na tukio fulani litakaloambatana na kuja huko kwa Roho Mtakatifu. Hawakuwa wakichukua sauti isiyojulikana. Bali walipohisi kitu fulani hicho kikisogea, na kuona ushahidi wa Biblia ukiambatana nacho, hawakuwa na tashwishi. Moja kwa moja wakaingia mitaani. Samahani. Loo, jamani! Walikuwa na hakika ilikuwa ni Roho Mtakatifu.

221 Unajua jinsi walivyokuwa na uhakika? Mpaka, Petro, maskini jamaa huyo asiye na elimu, akaruka juu kwenye kisiki ama kijisanduku, ama mahali fulani, kasema, "Enyi watu wa Yuda," maskini kifua mbele kama jogoo mkubwa. Akasema, "Ninyi watu wa Yuda, ninyi mnaoishi Yerusalemu! Nilikuwa nikiwaogopa, muda mfupi uliopita; siwaogopi, sasa. Hii na ijulikane kwenu, na myasikilize maneno yangu. Watu hawa hawajalewa kama mnavyodhania. Bali hili *ni* Lile." "Ati *tunatumaini* hili ni Lile"? "*Tunaamini* hili ni Lile"? Yeye alisema, "Hili *ni* Lile lililonenwa na nabii Yoeli." Haleluya! Hakuna tashwishi yoyote kulihusu. "Hili *ni* Lile lililonenwa na nabii Yoeli." Loo, jamani!

222 Yesu alisema, katika Marko 16, akaliagiza Kanisa Lake, "Enendeni ulimwenguni kote, mkaihubiri Injili." "Ati ishara hizi labda zinapaswa; zitafuatana, mara moja moja, labda"? "Zitafuatana na hao waaminio. Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio. Katika Jina Langu watatoa pepo. Watanena kwa lugha mpya. Wakishika nyoka au kunywa kitu cha kufisha, hakitawadhuru. Wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya." Sio, "Labda." "Watafanya. Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio."

223 Hebu niumalizie, katika kusema hili, ndugu, dada, kwa dakika chache zijazo. Ninaamini hilo. Ninaanimi ya kwamba kila kitu kingine, chochote kilicho kinyume na Hilo, si sahihi.

Ninaamini, kila kitu kinyume na Hilo kitaanguka. Ninaamini, sijali ni ukomunisti ngapi, ama ni itikadi ngapi *hizi* na itikadi *zile*, na ukanisa na Urumi, na zingine zote, Umarekani na chochote kingine kitaanguka.

224 Bali Neno hilo litasimama Milele, kwa kuwa ni Neno. Na kabla halijakuwa Neno, halina budi kuwa ni wazo. Nalo neno ni wazo lililotamkwa. Naye Mungu, katika Umilele, liliingia niani Mwake. Yeye aliyatamka mawazo Yake. Yakawa Neno, nalo Neno halina budi kudhihirishwa.

225 Hiyo ndiyo sababu, wakati Yeye aliponena juu ya Masihi, ilibidi Masihi atokee. Alinena kwamba kungekuwako na Kanisa katika siku za mwisho, lisilo na waa wala kunyanzi juu yake; kutakuwako na Kanisa pale. Haleluya! Alisema jambo hilo. Ninaliamini Neno Lake. Ninaliamini.

226 Ninaamini ya kwamba Yeye alimwahidi Roho Mtakatifu kwa kila mwaminio ambaye angeamini. Ninaamini Petro, kwenye Siku ya Pentekoste, wakati alipohubiri yale mahubiri muhimu, na kuwaambia wote watubu na kubatizwa, kwamba ishara hizi zingekuja, na *hili*. "Kila aliyeliitia Jina la Bwana angeokoka." Ninaamini hilo ni Kweli; kasimama juu yake. Nimeliona likidhihirishwa.

227 Ninajua ninalipigania. Nami najua ninajaribu kufanya wayo wa mguu. Kabla sijafanya wayo wa mguu, sina budi kukatilia mbali kila mfungamano, waridi mwitu, kila kitu kingine, kukiondoa njiani. Lakini kila unapopiga hatua, unasonga mbele. Amina. Chukua tu kisu na kuyakata.

228 Wengi wenu mnamkumbuka Paul Rader, rafiki wa thamani sana. Nilikuwa tu mvulana mhubiri, mtoto. Nilikuwa nimezoea kupanda kwenda Fort Wayne, kumsikiliza, kwenye Maskani ya Rediger. Jamaa mkubwa mno! Angerudi huko nyuma kabisa, avute suruali yake ndefu juu, ainue mkono wake na kunguruma kama dubu, nami ningewazia ataruka kupitia mimbarani. Wakati angeninii...Naye angeanza na fungu, naam, katika Mwanzo, na kumalizia katika Ufunuo, kote mbele na nyuma. Paul alikuwa mtu kwelikweli.

229 Akinena siku moja, yeye alisema, "Nilikuwa mkata miti huko Oregon," mahali alikotoka. Kasema, "Siku moja, mwajua," yeye alisema, "Ni—nilikuwa tu kwenye huduma ya umishenari, mbali sana mahali fulani." Ninasahau sasa mahali ilipokuwa. Naye alikuwa akifanya kazi ya umishenari.

230 Alimwamini Mungu, aliamini katika uponyaji wa Kiungu. Naye Paul akasema, papa hapa ambapo kanisa la ulimwengu linasimama siku hizi, yeye akasema, "Kama ningaliuuza ujumbe wangu wa neema kwa Wapentekoste waliowaka moto sana, badala ya kufanya yale nimefanya hapa nanyi kundi," kasema, "na kunifanya nihofu, nikaitwa mahali penye deni la maelfu mara maelfu ya dola. Nimehofu mpaka nikashikwa na kansa,

na sasa nafa. Kama ningaliuuza ujumbe wangu wa neema kwa Wapentekoste waliowaka moto sana, Mungu angalinibariki mno kwa ajili yake." Kweli.

231 Yeye alisema alikuwa huko chini katika—katika misitu, naye akashikwa na homa ya maji meusi ama kitu fulani. Ilikuwa mbaya sana. Naye alikuwa huko mbali misituni, na mwaminio hodari katika uponyaji wa Kiungu. Basi akasema aliendelea kuwa mgonjwa zaidi na zaidi. Aliomba, akaomba. Ndipo baadhi ya wamishenari wakasema walikuwa tu wanaenda kuchukua mtumbwi na kuleta daktari. Mbona, ingewachukua siku kadhaa kumfikia daktari. Naye akasema, "Mimi—mimi . . . Msifanye hivyo. Achaneni tu nalo." Kasema, "Mungu asiponiponya, basi naja Nyumbani."

232 Kwa hiyo akasema mke wake alikaa chumbani pamoja naye. Ikaendelea kuingia giza zaidi na zaidi. Basi akasema alimwita mke wake, kasema, "Mpenzi, ushike mkono wangu." Kasema, "Endelea tu kuniombea. Giza linaingia sasa." Kasema, "Ni—ninaamini vivuli vinaanguka kunizunguka." Akasema, "Shika . . . Ushike tu mkono wangu na kuomba, ninapoondoka." Akajikaza, kukutana na Mungu.

233 Kwa namna fulani akaingia katika usingizi mwepesi. Basi akasema aliota kwamba alikuwa amerudi hapa Oregon tena, kama kijana mwanamume, akikata miti. Na akasema bosi wa kambi alisema, "Paul, panda hapa upande fulani wa kilima, ukakate mti fulani, ukubwa fulani."

234 Alisema alikwea upesi juu ya hicho kilima kwa miguu yake ya ujana, akauangusha huo mti, akaupogoa, akaupigilia shoka. Alisema jinsi huo msonobari mwororo, shoka lake kubwa, kali, lenye kekee maradufu liliingia kwenye huo msonobari vizuri sana. Naye akasema aliushika, akawaza, "Vema, nitaubeba tu nishuke kilimani."

235 Mtu mzuri, mwenye nguvu, kasema, "Nilikuwa nikijizoeza jinsi ya kuweka magoti yangu pamoja, na kuunyanyua kwa mgongo wangu, sehemu iliyo kubwa zaidi ya mwanadamu." Misuli yake ilikuwa mgongoni mwake na mabegani, nyuma ya miguu yake. Kasema, "Ningeweza kulinyanyua gogo kubwa," akaliweka mgongoni mwake, akaondoka. Lakini kasema, "Hilo lilikuwa ni gogo la kawaida tu, lakini," kasema, "Mimi tu . . . " [Ndugu Branham anagonga maikrofoni—Mh.] Samahani. Kasema, "Kamwe singeweza kabisa kulisogeza gogo hilo." Nasikitika.

236 Akasema, "Kamwe nisingeweza kulisogeza gogo hilo." Akasema, "Nilipambana vikali, na kupambana na kujaribu kulinyanyua, na kabisa nisingeweza kufanya hivyo." Akasema, "Nilitoa nguvu zangu zote ndani yangu." Akasema, "Nisingeweza kabisa kulisogeza gogo hilo." Kisha kasema, "Hatimaye, nikadhoofika sana, nikaketi tu chini kuuegemea

huo mti na kuanza kufuta jasho. Nilikuwa nimedhoofika tu kabisa."

237 Na akasema, "Baada ya kitambo kidogo, nikasikia sauti ya bosi wangu." Lakini kasema, "Ilikuwa ni sauti iliyo tamu kuliko zote niliyopata kusikia." Tena kasema, "Nilipogeuka, sauti hiyo ikaniambia, 'Paul.' Nami nikasema, 'Naam, bosi, kuna nini?' Kasema, 'Kwa nini unalivuta kwa nguvu hivi?'" Akasema, "'Vema, uliniagiza kulileta huko chini kwenye kambi, nami nimejichosha kabisa, nalo. Kamwe—kamwe siwezi kulinyanyua, bosi.' Akasema, 'Paul, hivi huoni kile kijito cha maji kinachotiririka moja kwa moja *pale*?' Kasema, 'Naam.' Kasema, 'Kijito hicho huja moja kwa moja kambini. Kwa nini usilitupe tu majini, uruke juu yake na uliendeshe ushuke uje nalo kambini?' Kasema, 'Kamwe sikuwazia hilo.'"

238 Kwa hiyo akalibingirisha tu majini, akaruka juu yake, kasema, "Loo, jamani!" Akaanza kuyapiga maji, na kurukaruka, na kupiga mayowe, kwa sauti yake yote, huku akiyaabiri mawimbi, na kupitia majini, kila kitu, akiliendesha gogo hili, akishuka chini, akipiga makelele, "Ninaliendesha! Ninaliendesha!"

239 Akasema, muda si muda, akajirudia, alikuwa moja kwa moja katikati ya sakafu, huku mke wake akipiga mayowe pamoja naye. Angepiga makelele, "Ninaliendesha! Ninaliendesha! Ninaliendesha!" Ndugu!

> Mataifa yanavunjika, Israeli inaamka,
> Ishara ambazo Biblia ilitabiri;
> Siku za mataifa zimehesabiwa, zimekumbwa
>   na hofu.
> "Rudini, Enyi mliotawanyika, makwenu."

240 Ujumbe huu wa Neno la Mungu ni Kweli. Niishi nife, ninauendesha. Sininii . . . Sibishani na Huo. Sijaribu kubishana kuuhusu. Niliuchukua tu, nami ninauendesha. Acheni wakosoaji wainuke. Nitapiga kila bunduki kubwa. Naja kambini, moja ya siku hizi, nikiliendesha Neno la Mungu. Amina. Nina uhakika wa kuwasili kule.

Na tuombe.

241 Kwa nini uvutane na mzigo wako wa dhambi? Kwa nini uwe katika hali uliyomo, hujui unakosimama, ukikimbia kutoka kanisa moja hadi lingine, na mahali hadi mahali? Mbona usiurushe tu ndani, msalabani, usiku wa leo, na uendeshe juu ya Neno? Mbona usichukue tu ahadi ya Mungu usiku wa leo na uendeshe utoke kwenye haya machafuko, utoke uingie kwenye mbingu za samawati, zilizo wazi namna hiyo? Usivutane na Hilo. Usihofu na Hilo. Liamini tu, likubali. Ni Ufalme usioweza kutikisika. Liendeshe.

242 Kama wewe ni mgonjwa usiku wa leo, ichukue ahadi ya Mungu, "Mimi ni Bwana niyaponyaye magonjwa yako yote."

243 "Nitapataje kupona, Ndugu Branham? Daktari anasema nina ugonjwa wa moyo, nina kansa, nina *huu, ule*, wowote ule. Mimi ni kiziwi, bubu. Mimi ni kipofu." Nini, inaleta tofauti gani? Ikubali tu ahadi ya Mungu na uiendeshe.

244 Hebu na tuchukue fimbo kubwa mno, na kuishindilia hapa chini, na kuandika juu yake, "Maombi ya imani yameombwa usiku wa leo; nitayaendesha. Biblia ilisema, 'Kule kuomba kwa imani kutamwokoa mgonjwa, na Mungu atamwinua. Kama ametenda dhambi, atasamehewa.' Ninaendesha juu yake. Ninaliamini."

245 Kama umefanya makosa, kama u mkaidi usiku wa leo, "Yeye azifunikaye dhambi zake hatafanikiwa. Lakini yeye atakayezitubu dhambi zake atapata rehema." Kwa nini usiziungame?

"Vema, nifanye nini, Ndugu Branham?"

246 Ziungame, kisha uliendeshe. Mungu alisema hivyo. Litakuondoa moja kwa moja kutoka dhambini mwako.

247 Mtu huyo yupo hapa usiku wa leo, ambao kamwe hawajapata kuweka tumaini lao halisi ndani ya Mungu kwa ajili ya wokovu wa nafsi yako, nawe ungetaka kukumbukwa katika maombi tunapofunga? Waweza tu kuinua mkono wako, useme, "Niombee, Ndugu Branham. Ninataka kutupilia mbali shughuli zangu." Mungu akubariki. Mungu akubariki. "Nataka kutupa . . . " Mungu akubariki, mama. "Nataka kutupa shughuli zangu." Mungu akubariki, ndugu. Mungu akubariki huko nyuma, bwana. Mungu akubariki, msichana. Vema. Hiyo ni sawa. Mungu akubariki. "Nataka kutupa shughuli zangu juu Yake na kuendesha juu ya ahadi Yake sasa. Ninaamini kwamba Yeye aliahidi, 'Yeye atakayekuja Kwangu, sitamtupa nje kamwe.'"

248 "Sio jinsi ninavyojisikia, 'Niliombewa jana usiku, Ndugu Branham; sijisikii vizuri hata.'" Hilo halina uhusiano wowote nalo. Siendeshi juu ya hisia zangu. Ninaendesha juu ya Neno Lake. Ni ahadi Yake.

249 "Ndugu Branham, nimekuwa madhabahuni, mara nne ama tano, nikijaribu kumpokea Roho Mtakatifu. Kamwe sijampokea."

250 Hilo halimaanishi hata kitu kimoja. Kaa tu kwenye hilo gogo, litakuleta moja kwa moja kambini, katika kambi ya Mzaliwa wa Kwanza, katika kambi ya watakatifu. Utafika kule. Kaa tu kwenye gogo lako, na kupiga mayowe na kumsifu Mungu kwa nguvu uwezavyo. Hiyo ndiyo njia ya kufanya jambo hilo.

251 Wakati vichwa vyetu vimeinamishwa, kweli unataka kuliendesha? Basi, hicho kitu kidogo kinachogongagonga moyoni mwako, ungetaka kuja hapa na kusimama mbele ya

madhabahu kwa dakika moja? Na tuombe na kukuwekea mikono. Tungefurahia kama ukija.

252 Hebu na tuchukue hicho kitu kidogo kilichowekwa moyoni mwako usiku wa leo, na kusema, “Unajua, umekosea. Sasa inua mkono wako.” Vema.

253 Ulikanyaga lile gogo, gogo la ahadi Yake; ule mti, ule msalaba uliokatwa ukaanguka. Ukumbatie msalaba huu sasa. Tembea moja kwa moja hapa na kusema, “Sasa nitauendesha. Sasa hivi nitaliamini. Nitalikubali. Ninaliamini. Kamwe sitabadilika. Nitadumu moja kwa moja na Neno hilo, mpaka hilo limethibitishwa. Halafu basi baada ya hilo kuthibitishwa, nitanyosha mkono na kulichukua lingine, na kuanza kuliendesha moja kwa moja.” Mnaona?

254 Na neno kwa neno, hatua kwa hatua, utamiliki kila kitu ambacho Mungu alikuahidi. “Kwa maana mambo yote yanawezekana,” kwake atakeyeliendesha. Endesha juu ya ahadi Yake, kwa kuwa bila shaka itakuleta kambini. Itakuleta Mbele za Mungu.

255 Utakuja sasa wakati tumeviinamisha vichwa vyetu? Na kumwuliza yeyote ambaye angetaka kusimama madhabahuni, kwa muda kidogo tu wa maombi.

256 “Ninaliendesha, Bwana. Bwana, ninaamini. Mashaka yangu yote yemezikwa katika ile chemchemi. Bwana, naja. Ninaamini hilo. Ninasimama moja kwa moja juu ya Neno usiku wa leo, nami nitaliamini kwa moyo wangu wote. Ninaliamini Neno Lako.”

257 Mwanamke mmoja wa thamani amesimama hapa madhabahuni, ku—kumthibitishia Mungu kwamba yeye anamaanisha. Hivi si mje, mliokuwa mmeinamisha vichwa vyenu, na kuinua mikono yenu, na mlitaka kukumbukwa katika maombi? Mwaweza kuja tu hapa juu? Mungu awabariki. Njoni tu huku. Jambo ndilo hilo. Njoni moja kwa moja huku na kusimama hapa. Semeni, “Nitaliendesha. Mungu, Wewe ulifanya ahadi, kitu fulani kikaubisha moyo wangu, nami naja sasa hivi kuendesha juu ya hilo. Na nitakaa moja kwa moja juu yake mpaka linilete papo hapo kambini. Ninashuka moja kwa moja kwenye kambi ya watakatifu wa Aliye Juu kuliko wote.” Mungu akubariki. Hilo ni jema. Njoni moja kwa moja sasa, ninyi mnaotaka kuliendesha. Jinsi tu mlivyo, “Jinsi tu nilivyo, pasipo na kujitetea kamwe.”

258 Kumbukeni. Mnasema, “Huo ni mti?” Naam. Kulikuwako na mti uliokatwa, wakati mmoja, nao ukawekwa tena pale Kalvari. Urukie tu mti huo usiku wa leo, pamoja na ahadi za Mungu, lile Neno lililokuwa limetundikwa mtini.

259 Ninaliendesha. Nitaliamini, kwa moyo wangu wote. Ninataka kufanya kadiri ya kuja hapa na kupeana mikono na ndugu zangu.

260 Mungu awabariki, kwa ajili ya msimamo wenu imara. Ninataka mkae hapa, kwa muda kidogo tu, tunapoomba. Mungu akubariki, ndugu yangu. Dada yangu wa thamani, Mungu akubariki. Bwana Yesu . . . ?. . . Mungu akubariki, ndugu yangu. Mungu akubariki, dada. "Niongoze." Akuongoze kuvuka mto.

261 Kumbukeni, kama mtumishi wa Kristo, ninawajibika kwa kuhubiriwa kwa Neno. Ninawajibika kwa ushuhuda wangu. Nami hivi ningesimama hapa usiku wa leo . . .

262 Na mtu mwenye umri wa miaka hamsini na mitano, ama umri wa miaka hamsini na mitatu, nitakuwa na hamsini na minne mnamo Aprili, na kusimama hapa na kujua ya kwamba, hata ono hili la mwisho, huenda zikawa ndizo siku zangu chache za mwisho duniani. Hu—huenda nikawaacha katika siku chache. Sijui maana yake. Sikiliza tu hiyo kanda na utoe maamuzi yako mwenyewe. Sijui maana yake. Hivi ningesimama hapa, nikiamini nusu kwamba huenda ikawa ndizo jumbe zangu za mwisho nitakazopata kuhubiri, ni papa hapa Phoenix, na kusema jambo lisilo sahihi, na kujua kwamba ukomo wangu uko kule ng'ambo, nami nitahukumiwa kwa maneno yangu?

263 Ndugu zangu, hebu niwaambieni hili, na dada zangu. Mmekuwa kwenye mikutano. Mnajua nini, ule upambanuzi na kadhalika. Hivi nimewahi kuwaambia lolote, katika Jina la Bwana, ila lile lililotimia? Nitamwuliza mtu yeyote. La, bwana. Kote ulimwenguni, na maelfu ya maono, kamwe hapajakuwapo. Nami nawaambia ukweli usiku wa leo, Damu ya Yesu Kristo imetosha kabisa hata inaondolea mbali kila waa, nayo ingetosha.

> Kuna chemchemi iliyojaa Damu.

Nanyi mnasimama kwenye Hiyo sasa.

> Iliyotolewa kwenye mishipa ya Imanueli,

Kitu pekee cha hakika kilichosalia duniani.

> Ambapo wenye dhambi wakitumbukia katika gharika hiyo,
> Hupoteza waa lao lote la dhambi.

264 Nitawaomba hawa wahudumu sasa, na ndugu, kama mtakuja hapa miongoni mwa watu hawa. Yeyote yule aliye . . . Hivyo ndivyo, mnavyowaita wahudumu kuomba pamoja na watu? Wahudumu wote hapa ndani, basi, wanaotaka, wanaovutiwa kuwaona watu wakiokoka, njoni hapa na kusimama kama kundi la waombaji, ambapo tunaweza kujifunga pamoja, kuyaondokea mengine yote, na kujitenga. Hawa ni wanaume na wanawake wanaotia muhuri kikomo chao, usiku wa leo, kwa Damu ya Yesu Kristo, wakiamini Neno Lake, wakiendesha hata kuingia katika Uwepo Wake, juu ya Neno Lake, na kusema, "Mimi hapa, Bwana. Sina kitu cha kutoa ila nafsi yangu, na unichukue." Hivi mtakuja na kusimama pamoja

nao, mkipenda? Mtu yeyote anayetaka kuja, njoo usimame. Mungu awabariki, ndugu zangu. Hilo ni zuri mno. Ninapenda kuona watu walio hodari, wanaojali nafsi. Nadhani, ndugu zangu, hilo ni jema. Njoni moja kwa moja karibu. Hilo ni zuri. Simameni huku. Hebu sasa hivi . . .

265 Kama mpiga piano ataenda kwenye muziki, akipenda, hebu tuimbe wimbo huu, kwa utamu sasa, kwa utimamu, uchaji.

266 Tunakuja sio kwa kitu fulani cha kubuni. Hatuji kwa kitu fulani ambacho ni i—i—imani tu ya kujifanya. Bali tunakuja katika Uwepo wa Mungu, Yehova Mungu mwenye nguvu zote, Yule aliahidi, kwamba, "Popote wawili au watatu wamekusanyika katika Jina Langu, hapo nipo miongoni mwao." Zungumza na Yeye kama vile ungezungumza na rafiki yako, useme, "Bwana, samahani. Nimetenda dhambi." Nasi tunaenda kuimba.

Kuna Chemchemi iliyojaa Damu,
Iliyotolewa kwenye mishipa ya Imanueli,
Ambapo wenye dhambi wakitumbukia chini
ya hiyo Gharika,
Hupoteza waa lao lote la dhambi.

Mwizi yule aliyekuwa akifa alifurahia kuona
Chemichemi hiyo katika siku yake;
Hapo nijalie mimi, ingawa ni mwovu kama
yeye,
Nioshe na kuondolea mbali dhambi zangu
zote.

Tangu hapo kwa imani nilipokiona kile Kijito
Kilichotoka kwenye majeraha Yako,
Upendo wa ukombozi umekuwa ndio wimbo
wangu,
Na utakuwa hivyo mpaka nitakapokufa.

267 Iweni tu wadogo sana sasa. Wewe si kitu. Hakuna mmoja wetu asiye kitu. Na kwa uaminifu tu sasa, kwa mioyo yenu yote, inamisheni tu mioyo yenu na vichwa vyenu, kila mahali, kote jengoni.

268 Baba yetu wa Mbinguni, ninajua ya kwamba Maneno Yako ni ya kweli kabisa. Hayawezi kushindwa. Ni Neno la Mungu. Hayo ni Mungu. Na Wewe ulisema, "Yeye anijiaye Mimi, sitamtupa nje kamwe." Nao wanaume hawa na wanawake, chini ya imani, wakijua kwamba hawako sawa, wamekuja mbele, usiku wa leo, Bwana, kukiri kwamba wamekosea, wakijua ya kwamba wamepata mdundo kwa mhemko fulani wa ndani ambao—ambao uliwaalika waje kwenye Chemchemi. Nao hapa wamesimama, na vichwa vilivyoinamishwa pamoja na mioyo, kuyanywa maji ya Uzima, bure, yaliyoahidiwa na Mungu. Wapokee, Baba, katika Ufalme Wako. Hao ni Wako.

269 Wewe ulisema, “Hakuna mtu awezaye kuja Kwangu asipovutwa na Baba Yangu kwanza. Na wote ambao Baba amenipa Mimi watakuja Kwangu.” Nayo inaonyesha kwamba Mungu amempa Kristo hawa, kama zawadi ya upendo. Nao hawa hapa wamesimama, Bwana. “Hakuna mtu anayeweza kuwatoa mkononi Mwangu.” Nami naomba, Mungu, ya kwamba Wewe utawaweka salama usiku wa leo, wanaposimama hapa, na uwape ubatizo wa Roho Mtakatifu wakati wakiwa hapa madhabahuni.

270 Jalia nguvu kuu za Kristo ziyaloweshe sana maisha yao sasa! Walifanya maungamo yao. Walisonga mbele. Wewe ulisema, “Yeye atakayenikiri Mimi mbele za watu, huyo nitamkiri mbele za Baba Yangu na Malaika watakatifu.” Tunajua kazi hiyo inafanywa.

271 Sasa, Bwana, watie muhuri katika Ufalme wa ahadi, wa Roho Mtakatifu. Tujalie, Bwana. Imwage Roho Yako juu yao, na uwajaze kwa Roho wa Mungu aliye hai, wapate kuwa shuhuda zilizo hai siku zote za maisha yao, kwa Ufalme wa Mungu.

272 Sasa hebu na kusanyiko lisimame. Kila mtu katika maombi sasa. Tutaomba kwamba hawa . . .

273 Sasa, kila mmoja wenu aliyekuja hapa usiku wa leo, ukijisikia ya kwamba ulikuwa na dhambi moyoni mwako, sasa hakuna kitu unachoweza kufanya ila kuamini hilo. Mtakatifu . . . Unalikubali *Hili* kwa imani. Hii ni imani, unayoikubali. Yesu alisema, “Hakuna mtu awezaye kuja Kwangu asipovutwa na Baba Yangu kwanza. Na wote wanijiao Mimi,” Yeye atawapokea. Hawezi kufanya lingine lolote, kwa sababu Yeye aliliahidi. Mnaona? Usitulie juu ya mhemko sasa. Tulia juu ya Neno Lake. Unaona? Neno lilisema hivyo.

274 “Yeye ayasikiaye Maneno Yangu na kumwamini Yeye aliyenipeleka, yuna,” wakati uliopo, “Uzima wa milele, wala hataingia Hukumuni, bali amepita kutoka mautini kuingia Uzimani.” Roho Mtakatifu ni tukio la kujazwa na kuvikwa nguvu kwa ajili ya utumishi. Bali maungamo na kumpokea Kristo ni kuwa na imani na kufanya maungamo yako, na kujisikia huru kwamba Mungu amekusamehe dhambi zako.

275 Na juu ya msingi wa Neno Lake, Yeye alisema, “Hakuna mtu awezaye kuja asipovutwa na Baba Yangu kwanza.” Mnaona? Sasa, Mungu alikuvuta, kwanza. “Na yeye atakayekuja Kwangu, sitamtupa nje kamwe.” Mnaona? Mnaona? Wewe, umelipokea. Jambo pekee, una ninii . . .

276 Yeye, alikufa kwa ajili yako. Dhambi zako zilisamehewa, miaka elfu moja mia tisa iliyopita. Umekuja tu sasa kukubali yale aliyokufanyia. Unaona? Na wewe unaamini kwamba Yeye alikufa kwa ajili ya dhambi zako? Utamkubali kama upatanisho wako? Kwa maneno mengine, mkubali Yeye, kwa kuwa Yeye alizichukua dhambi zako.

277 Utafurahi na kumshukuru Yeye kwa kuzichukua dhambi zako? Unaamini Yeye alizichukua? Basi inua tu mkono wako, useme, "Ninaamini ya kwamba Yeye huichukua dhambi yangu," amina, "huichukua dhambi yangu." Vema.

278 Sasa, wewe sasa ni mtarajiwa kwa ajili ya ubatizo wa Roho Mtakatifu.

279 Endapo hujaupokea ubatizo wa Kikristo, mmoja wa watu hawa hapa atashughulikia hilo, kwamba upate ubatizo wa Kikristo.

280 "Lakini sasa Petro alipokuwa akisema maneno haya, kabla hawajabatizwa; Petro alipokuwa akisema maneno haya, Roho Mtakatifu akawashukia." Kwa nini? Wote walikuwa chini ya matarajio. Sasa ninyi mko chini ya matarajio. Mnataka kitu fulani sasa kitakacho—kitakachowatia muhuri katika Ufalme wa Mungu, kitu kitakachokuwa halisi kwenu. Mnataka kupo-. . .Hivi hamtaki kumpokea Roho Mtakatifu, kila mmoja wenu? Hivi hamumtaki? Hakika, mnamtaka. Hizo ndizo nguvu zenu za kuwadumisha. Mnaona?

> Walikuwa wamekusanyika katika chumba cha juu,
> Wakiomba katika Jina Lake, ninii . . .
> Walibatizwa kwa Roho Mtakatifu,
> Ndipo nguvu za huduma zikaja.

281 Mnaona? Loo, hilo ndilo mnalotaka sasa. Nanyi mnaweza kulipata, sasa hivi. Ni kwa ajili yenu, sasa hivi.

282 Sasa, ndugu zangu, njoni huku. Hebu, kila mmoja sasa, na tuweke mikono yetu juu ya ndugu hawa, na tuombe kwamba wampokee Roho Mtakatifu. Njoni moja kwa moja huku, ndugu. Pandeni moja kwa moja huku.

283 Sasa, kusanyiko lote, inueni mikono yenu sasa, kila mtu! . . .? . . .

284 Baba yetu wa Mbinguni, katika Jina la Bwana Yesu Kristo, jaza kila moyo hapa kwa ubatizo wa Roho Mtakatifu.

285 Mpokeeni Roho Mtakatifu. Mpokeeni Roho Mtakatifu, watu hawa hapa wanaosimama na kuungojea ule Uwepo na nguvu za Mungu ziyaloweshe maisha yao.

Baragumu Ikitoa Sauti Isiyojulikana SWA63-0114
(A Trumpet Gives An Uncertain Sound)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, uliotolewa hapo awali katika Kiingereza Jumatatu jioni, tarehe 14 Januari, 1963, kwenye Kusanyiko la Kikristo huko Phoenix, Arizona, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2020 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org